# ATHARI ZA TEKNOLOJIA KATIKA NGANO

**Na**

**Maimuna Ali Mbarouk**

**Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma**

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**Oktoba, 2015**

## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayohusu *Athari za Teknolojia katika Ngano* na kupendekeza ipokelewe na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa azma ya kutimiza masharti ya mahitaji ya kumaliza shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma, kwa idhini ya msimamizi aliyeteuliwa rasmi na uongozi wa chuo.

…………………………………………………………….

Dkt Muhammed Seif Khatib

Msimamizi

Tarehe …………………………………………..

**IKIRARI**

**NA**

**HAKIMILIKI**

Mimi, **Maimuna Ali Mbarouk** nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na mtu mwengine yeyote katika chuo kingine chochote au Baraza lolote la Chuo Kikuu ama mabaraza mengine kwa lengo la kupata Shahada ya Uzamili.

Sahihi…………………

Hairuhusiwi kuzalisha, kutafsiri, kunakiri, kupiga chapa, kuiga na wala kusambaza sehemu yeyote ya tasinifu hii kwa namna yeyote ile bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## SHUKRANI

Sina budi kumshukuru Allah (S.W) muumba mbingu, ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Yeye ndiye aliyenijaaliya uzima, afya pamoja na kunipa maarifa ya kuweza kukamilisha utafiti huu.

Kwanza, natoa shukrani za dhati kwa msimamizi wangu Dkt. Muhammed Seif Khatib ambaye alijitolea kuniongoza na kunisimamia kwa kunipa mawazo, fikra pamoja na mwongozo wake ndiyo ulionisaidia na kunipa msukumo wa kufanya kazi hii na kufikia kiwango hiki nilichofikia.

Pili, napenda kumshukuru dada yangu mpenzi Fatma Ali Mbarouk kwa kunivumilia na kunitunzia familia yangu vizuri katika kipindi kigumu cha masomo mpaka kukamilisha utafiti huu. Pia nawashukuru ndugu zangu Naima Ali na Asha Ali kwa kushirikiana na mlezi katika kuitunza familia yangu wakati wa masomo.Vile vile nawashukuru wanangu Yumnah, Rashid, Zinnira, Uzeir na Dhalkarnain kwa kuvumilia na kukosa mapenzi ya mama yao kwa kipindi chote cha masomo.

Tatu, nawashukuru wazazi wangu Bi Fatma Khamis Juma na Bw Ali Mbarouk Salim kwa kuelewa umuhimu wa elimu na kunipeleka skuli na kufika hapa nilipo. Mungu awalipe kheri duniani na kesho akhera.

Mwisho nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitomshukuru mume wangu Ali Rashid Hassan kwa kunisaidia kwa hali na mali na kunivumilia katika kipindi chote cha masomo na kuikamilisha kazi hii kama hivi ilivyo. Allah amfungulie milango ya kheri na Baraka.

## TUNUKU

Naitunuku kazi hii kwa baba yangu Bw Ali Mbarouk, mama yangu Bi Fatma Khamis Juma na mume wangu mpendwa Ali Rashid Hassan. Allah awape afya iliyo njema in shaa Allah.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza Athari za Teknolojia katika Ngano, ambao uliongozwa na malengo matatu nayo ni kuchunguza historia ya ngano Zanzibar, kuchambua maendeleo ya teknolojia ambayo yanaathiri ngano na kubainisha athari za maendeleo ya teknolojia katika hadithi za ngano.

Mbinu zilizotumika ili kuweza kutatua tatizo la utafiti ni udurusu wa kimaktaba, usikilizaji wa vyombo vya habari, mahojiano na mjadala wa vikundi. Sampuli ya watafitiwa ilikuwa ni wanafunzi, walimu kutoka SUZA, wakaazi wa mkoa wa Mjini Magharibi na wafanyakazi wa ZBC. Nadharia aliyotumia mtafiti katika uchambuzi wa data ni nadharia ya uhalisia ambayo ndiyo iliyomuongoza katika uchambuzi wa data.

Matokeo yautafiti yanaonesha kuwa chimbuko la ngano ni kuwaasa watoto juu ya tabia ambazo hazikubaliki katika jamii, watu kujionesha kuwa wana vipawa vya kutumia lugha na pia ni watu kutaka kujionesha namna wanavyoyaelewa mazingira yao. Ngano ziliwasilishwa kwa mdomo. Maendeleo ya teknolojia ambayo yanatumika kuwasilishia, kuhifadhia, kusambaza ngano ni maandishi, CD, kanda za video na kanda za kunasia sauti pamoja na kompiyuta. Athari zinazopatikana kwa kutumia vifaa vya teknolojia katika kuwasilisha, kuhifahia na kusambazia ngano zimebainika kuwa zipo chanya na hasi.

Mwishowe utafiti huu umetoa mapendekezo kuwa serikali kupitia wizara husika kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa ngano na pia kuzikusanya kwa ajili ya kuzihifadhi ili zisipotee moja kwa moja, teknolojia ambayo itatumika kuhifadhia ngano hizo iwe ni ya kudumu na kuigizwa ili zipate uasili wake na pia maskulini sisitumike kufundishia lugha tu bali iwe ni nyenzo ya wanafunzi kuvuna taaluma iliyomo katika ngano hizo.

## YALIYOMO

ITHIBATI YA MSIMAMIZI ....................................................................................i
IKIRARI NA HAKIMILIKI .................................................................................. ii
SHUKRANI ........................................................................................................ iii
TUNUKU ............................................................................................................iv
IKISIRI...............................................................................................................v
YALIYOMO .......................................................................................................vi
VIAMBATANISHO ..............................................................................................ix
UFAFANUZI WA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAFITI.......................x
VIFUPISHO VYA MANENO.............................................................................. xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ....................................................................1**
1.1 Utangulizi..........................................................................................................1
1.2 Usuli wa Tatizo ..................................................................................................3
1.3 Tamko la Utafiti .................................................................................................5
1.4 Malengo ya Utafiti ............................................................................................6
1.4.1 Lengo la Jumla ................................................................................................6
1.4.2 Malengo Mahsusi .............................................................................................6
1.4.3 Maswali ya Utafiti............................................................................................6
1.5 Manufaa ya Utafiti ............................................................................................6
1.6 Nadharia ya Utafiti ............................................................................................6

**SURA YA PILI .....................................................................................................9**
2.0 Utangulizi...........................................................................................................9
2.1 Maandiko kuhusu Teknolojia.............................................................................9
2.2 Fasili ya Teknolojia ............................................................................................9
2.2.1 Nafasi ya Teknolojia katika Fasihi....................................................................9
2.2.2 Maandiko Kuhusu Maana na Sifa za Hadithi za Kimapokeo ...........................12
2.2.3 Historia ya Hadithi za Kimapokeo...................................................................13
2.2.4 Pengo la Utafiti ...............................................................................................14
2.2.5 Hitimisho.........................................................................................................15

**SURA YA TATU: USANIFU NA MBINU ZA KUKUSANYIA DATA ............16**
3.0 Utangulizi ............16
3.1 Mpango wa Utafiti ............16
3.2 Mkabala wa uchambuzi wa data ............16
3.3 Walengwa wa Utafiti ............16
3.3.1 Makundi tafitiwa ............17
3.3.2 Waalimu wa SUZA ............17
3.3.3 Wafanyakazi wa ZBC ............17
3.3.4 Wanafunzi wa Sekondari ............17
3.3.4 Wakazi wa Zanzibar ............17
3.4 Sampuli ya Watafitiwa ............18
3.4.1 Eneo la Utafiti ............19
3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ............19
3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data ............19
3.5.2 Udurusu wa Kimaktaba ............19
3.5.3 Usikilizaji wa vyombo vya Habari ............20
3.5.4 Mahojiano ............20
3.6 Vifaa na zana za kukusanyia data ............20
3.6.1 Kalamu, penseli na karatasi ............20
3.6.2 Simu ya Mkononi ............20
3.6.3 Redio na Televisheni ............20
3.6.4 Kompyuta ............21
3.7 Ukusanyaji wa Data na Udhibiti ............21
3.7.1 Mipaka ya utafiti ............21
3.7.2 Vikwazo vya Utafiti ............22
3.7.2.1 Uelewa Mdogo wa Dhana ya Ngano ............22
3.7.2.2 Urasimu katika Kupata taarifa katika Vyombo vya Habari ............22
3.7.2.3 Upungufu wa Fedha ............22
3.7.2.4 Ukosefu wa Vitabu ............23

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ............24**
4.0 Utangulizi ............24
4.1 Historia ya Fasihi katika Jamii ya Zanzibar ............24

4.2 Chimbuko na Asili ya Hadithi za ngao za Zanzibar ....27
4.3 Mfumo wa Ngano kabla ya maedeleo ya Teknolojia ....32
4.3.1 Utungaji wa Ngano ....33
4.3.2 Uwasilishaji ....34
4.3.3 Uhifadhi wa ngano ....35
4.3.4 Usambazaji ....36
4.3.5 Dhima ya ngano ....36
4.3.5.1 Kuelimisha ....36
4.3.5.2 Kuburudisha ....37
4.3.5.3 Kuasa ....37
4.3.5.4 Kurithisha Amali za Jamii ....38
4.4 Teknolojia Inayotumika Kuwasilisha, Kuhifadhi, na Kusambaza Ngano Zanzibar ....38
4.4.1 Redio ....39
4.4.2 Maandishi ....39
4.4.3 Kanda za video na CD ....41
4.4.4 Kompyuta ....41
4.5 Athari za Teknolojia katika Kutunga, Kuwasilisha, Kuhifadhi na Kusambaza Ngano ....41
4.5.1 Athari Chanya za teknolojia katika kuwasilisha, kuhifadhi, kusambaza na dhima za Ngano ....42
4.5.2 Athari hasi za Teknolojia katika Kuwasilisha, Kuhifadhi na Kusambaza Ngano ....45

**SURA YA TANO: HITIMISHO LA UTAFITI ....52**
5.1 Muhtasari wa Tasnifu ....52
5.2 Utoshelevu wa Nadharia ....53
5.3 Matokeo ya utafiti ....54
5.4 Mapendekezo ya Utafiti ....56
5.5 Mapendekezo Kuhusu tafiti Nyengine: ....56
**MAREJELEO ....58**
**VIAMBATANISHO ....60**

## VIAMBATANISHO

Kiambatanisho 1: Hadithi ya jongoo na nyoka ........................................................60
Kiambatanisho 2: Hadithi ya Mnara wa Baba na Mama ..........................................61
Kiambatanisho 3: Hadithi ya Mtendazema ................................................................67
Kiambatanisho 4: Hadithi ya Zimwi ...........................................................................70
Kiambatanisho 5: Hadithi ya Sungura na Buyu la Asali ...........................................72
Kiambatanisho 6: Kinyonga Mfalme wa Wanyama ..................................................74
Kiambatanisho 7: Hadithi ya Mcheka Kilema ...........................................................76

## UFAFANUZI WA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAFITI

**A) Ngano**

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) anasema "Ngano ni hadithi ya kale ambayo ni moja ya tanzu maarufu za fasihi simulizi. Ni moja kati ya vipera au vitanzu vya hadithi au simulizi. Ngano nyigi huwa na mwanzo wa "Hapo zamani za kale." Ngano hupokezwana katika jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

**b) Hadithi za Kimapokeo**

Haya ni masimulizi ambayo yanasimulia kuhusu ushujaa, historia ya jamii, ulafi, na uchoyo. Hadithi hizi ni za kale na zinarithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hadithi hizi ni za kubuni ambazo hutumia wahusika kama vile wanyama, mazimwi, binadamu na vitu vyengine. Wahusika hawa huyasawiri maisha ya jamii husika. Hii ni moja kati ya tanzu za fasihi simulizi.

**c) Fasihi Simulizi**

Hii ni fasihi ambayo huwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo. Hadhira na fanani huwa uso kwa uso pale inapowasilishwa.

**d) Maendeleo**

Maendeleo ni hali ya kutoka hatua moja ambayo ni duni kwenda hatua nyengine iliyo bora zaidi. Kwa mfano jamii huweza kutengeneza vitu kwa mikono ambapo mafanikio huwa madogo na kupiga hatua ya kutumia mashine na kupata mafanikiokatika utengenezaji huo.

**e) Athari**

Ni matokeo au mabadiliko yanayopatikana kwa kutumia kitu fulani kufanya jambo jengine. Mfano utumiaji wa madawa ya kulevya yanaweza kuleta athari ya kiafya kwa mtumiaji. Athari inaweza kuwa hasi au chanya.

**f) Teknolojia**

Kwa mujibu wa *Oxford Advanced Learners Dictionary* toleo la mwaka 2000 ukurasa 1230 neno teknolojia limetafsiriwa kuwa;

Teknolojia ni ule ujuzi, maarifa na elimu ya sayansi ambayo hutumika kimatendo (katika kiwanda) mfano kwa ajili ya kubuni mashine mpya. (Tafsiri yangu).

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Barasa la Kiswahili Zanzibar. |
| TAKILUKI | Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar. |
| SUZA | The State University of Zanzibar. |
| ZBC | Shirika la Utangazaji Zanzibar. |
| Bw | Bwana |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu wa **Athari za Teknolojia katika Ngano** umefanyika katika mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar. Ngano zikiwa ni hadithi za kale ni zao la jamii. Jamii hiyo huwa na shughuli za kibinadamu katika dunia tunayoishi vikiwemo visiwa. Zanzibar ni sehemu ya dunia ambayo wanajamii wake wanazo ngano zao zikiwa ni miongoni mwa tamaduni zao. Zanzibar ni mkusanyiko wa visiwa viwili, pamoja na visiwa vyengine vidogo vidogo katika mwambao wa Afrika Mashariki. Kijiografia, visiwa hivi vipo katika bahari ya Hindi takribani nyuzi 6 kusini mwa Ikweta (Else; 1993:1). Visiwa hivi ni Unguja ambacho kimezoeleka kuitwa Zanzibar na Pemba. Visiwa hivi vimezungukwa na bahari ya Hindi ambayo pepo zake za kusi na kaskazi zimewezesha kuwa na mwingiliano mkubwa wa wageni kutoka mabara mbalimbali duniani. Miongoni mwa wageni ambao waliingia katika visiwa hivi ni Waajemi, Waarabu, Wahindi, Wareno na Waingereza. Wageni hao walileta athari kubwa katika utamaduni, uchumi na siasa za watu wa jamii hizi. Jambo hili ni la kawaida kwani jamii yeyote hupata mabadiliko kutokana na mwingiliano wa watu na mabadiliko yeyote yanayotokea katika jamii. Visiwa vya Zanzibar vimezungukwa na bahari, hivyo basi uvuvi ni moja kati ya njia kuu za uchumi wake. Sambamba na hili, Wazanzibar hulima vyakula vya nafaka kama vile mpunga, mtama mahindi na uwele. Zao kuu la biashara ni karafuu ambazo zaidi hulimwa katika kisiwa cha Pemba. Kwasasa utalii ni moja kati ya njia zake za kuimarisha uchumi.

Watu wengi wa Zanzibar asili yao ni kutoka bara la Afrika ambao waliingia Zanzibar takriban miaka 5000 mpaka 6000 iliyopita (Else, 1993:3). Else anadai kuwa Waafrika hao asili yao ni Wabantu ambao walihama kutoka Afrika ya Kati

kuja kuishi Mashariki na Kusini mwa Afrika. Katika mwambao wa Afrika Mashariki, ikiwemo Zanzibar, watu wengi walichukua mila za Waarabu ambao walikuwa wakifanya biashara zao na baadae kutawala katika sehemu za mwambao. Watu hawa walitambuliwa kuwa ni Waswahili na lugha yao ni Kiswahili. Mchanganyiko wa watu wa Zanzibar na wegine kutoka nje ya Afrika, umeibua utamaduni changamano kama unavyoelezwa na Juma, (2008: 26) pale anaposema:

> *Kama ilivyo asili yao, utamaduni wa watu wa Zanzibar ni changamano. Una mengi yanayofanana na tamaduni za watu wanaoishi katika upwa wa Afrika Mashariki. Lakini hatuwezi kusema kuwa tamaduni hizi ni sawa sawa sahani na kawa. Kwa hali yeyote mipaka ya kijiografia haikosi kuacha athari katika tamaduni za watu wa maeneo haya licha ya kuwa na muhimili madhubuti wa lugha unaowaunganisha.*

Aidha, Khamis (2008: 1-22) katika makala yake *Jaadi na Utamaduni wa Mswahili wa Zanzibar* anadai kuwa Waswahili (Wazanzibar) wana utamaduni na jadi zao kama vile kuishi katika viambo, mitaa au vijiji. Watu wazima nao huwa wana michezo yao kama vile bao, karata na kadhalika. Wakati watoto wao wakiwa wakijishughulisha na michezo kama vile foliti, kutoleana hadithi na mengi mengineyo.

Waswahili wa visiwa hivi wengi wao ni Waislamu na asilimia ndogo ni Wakiristo. Waislamu hawa ni wa madhehebu ya Suni na Wakiristo ni wa madhehebu ya Anglikana. Pamoja na kujulikana kuwa ni Waswahili, watu wa Zanzibar wamegawika katika makundi makuu matatu. Wahadimu wapo waishiyo kusini na kati ya kisiwa cha Unguja. Watumbatu wapo katika kisiwa cha Tumbatu na

kaskazini ya Unguja na Wapemba wapo katika kisiwa cha Pemba. Pamoja na hao, pia yapo makundi ya jamii ya Magoa, Wahindi, na Waarabu.

Kisiwa cha Unguja kina mikoa mitatu ambayo ni Kusini, Kaskazini na Mjini Magharibi. Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo utafiti huu umefanyika ndiyo mji mkuu wa visiwa hivi. Ofisi za serikali, za watu binafsi na wageni wa aina mbalimbali kutoka maeneo tofauti duniani wanapatikana humu. Mjini Magharibi hasa Mji Mkongwe, ni sehemu ambayo imeanza kuwa kitovu cha utawala tangu enzi za tawala za jadi zilizokuwapo kabla ya ukoloni; ambapo makao makuu yalikuwa Forodhani kama anavyoeleza Juma (2007: 3); na hali hii inaendelea hadi leo. Katika mkoa huu shughuli mbalimbali za kijamii zinafanyika; kwa mfano biashara, usafirishaji na uingiaji wa abiria na bidhaa kutoka maeneo tofauti.

Kwa upande wa sanaa, mkoa huu umesheheni aina kwa aina za burudani. Watu hupata burudani kupitia televisheni, kompyuta, kutembelea viwanja vya michezo pamoja na kuangalia michezo iliyorikodiwa katika CD au tepurikoda. Uibukaji wa teknolojia ya kurikodia na kuhifadhia kazi mbali mbali za sanaa, fasihi simulizi ikiwemo, unaonekana kuleta athari katika jamii. Utambaji wa hadithi ya ngano ambao ulikuwa kivutio zamani umekumbwa na teknolojia hii na hivyo umeweza kuleta mabadiliko chanya na hasi.

## 1.2 Usuli wa Tatizo

Hadithi za kimapokeo (ngano) ni hadithi za masimulizi ambazo asili yake zinatokana na fasihi simulizi. Hadithi hizi zilitolewa kwa njia ya masimulizi bila ya kuandikwa, kwa hivyo hadhira na fanani huwa wanaonana na kushiriki katika matendo mbalimbali kama vile kuimba, kucheza na kupiga makofi. Hadithi hizi zilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya masimulizi. Hadithi hizi hasa

zilisimuliwa wakati wa usiku; wakati ambao watoto wanasubiri chakula cha jioni (chajio). Hali hii hulazimika kutokana na sababu kwamba wazazi ambao walikuwa ndiyo wasimuliaji wakuu wa hadithi hizo, huwa wakati huo wamerejea kutoka katika mahangaiko yao ya kujitafutia riziki ili kuwafanya watoto wasilale kwa ajili ya kusubiri chakula hadithi hutolewa kwao. Wakati wa mavuno ya karafuu huko Pemba, hadithi hizi zilisimuliwa kwa lengo la kuwashajiisha watoto kusaidia katika kazi ya uchambuzi wa zao hilo. Hadithi hizi zinapotolewa huwaburudisha watoto kwani ziliwashirikisha watoto kwa njia mbalimbali kama vile kuuliza maswali, kuimba na kadhalika. Na hapo watoto hujisisikia kushirikishwa kwao katika utambaji wa hadithi hizo.

Kabla ya maendeleo ya teknolojia, hadithi za kimapokeo zilikuwa na miundo maalum hasa katika mianzio na miishio yake, kama vile kuanza na neno “Paukwa-pakawa” na kuishia na “Waliishi raha mustarehe”. Ngano zilikuwa zikihifadhiwa kifuani na baadaye kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Maudhui ya hadithi hizi yalikuwa ni kuadilisha na kutahadharisha juu ya tabia mbaya.

Mabadiliko katika jamii yeyote ni jambo ambalo haliwezi kuzuilika katika kila uga wa maisha ya mwanadamu. Kadiri siku zinavyokwenda mwanadamu huvumbua mbinu mbalimbali za kumrahisishia utendaji wake wa kazi na kumburudisha. Uvumbuzi wa teknolojia unaonekana kuathiri jamii zetu katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Fasihi nayo imepata athari hizi kutokana na ukweli kwamba fasihi ni zao la jamii na kwa hivyo haina budi kufuata mabadiliko yaliyomo katika jamii. Kwa hivyo, bila shaka hadithi za kimapokeo, ikiwemo ngano zinaonekana kupata mabadiliko katika miundo, uwasilishwaji, uhifadhi na hata maudhui. Hali hii

ndiyo iliyomsukuma mtafiti kuchunguza namna maendeleo ya teknolojia yanavyoathiri ngano.

### 1.3 Tamko la Utafiti

Dhana ya ngano ikiwa ni miongono mwa tanzu za fasihi simulizi imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali, miongoni mwao ni Senkoro (2011: 53) ambaye anasema

> *Ngano ni utanzu wa kifasihi simulizi ambao ulipitishwa*
> *kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo.*
> *Utunzi wake, kinyume na hadithi tulizo nazo leo,*
> *haujulikani, wala hauewezi kuwa ni wa mtu huyu*
> *ama yule. Ubinafsi wa kiutungaji pamoja na umuhimu*
> *na ufahari wa mtungaji haukuwa na uzito tuonao leo.*

Kutokana na ukweli huu utungaji na utambaji wa hadithi za ngano umepata mabadliko kutokana na maendeleo ya teknolojia yaliyomo katika jamii zetu. Maendeleo ya teknolojia kama yale ya uandishi, vifaa vya kurikodia na kunasia sauti, kompiyuta na intaneti yameleta mabadiliko chanya na hasi katika hadithi za ngano.

Tafiti mbalimbali juu ya hadithi za ngano zimefanywa, hata hivyo, yawezekana kuwa zipo ambazo bado hazijashughulikia na kuona namna teknolojia inavyoziathiri hadithi hizo. Wataalamu wengi ambao wamefanya tafiti kuhusiana na utanzu huu, wamejikita zaidi katika kuangalia fani na maudhui. Hali hii, kwa upande mwengine, inawafanya wanajamii kutoelewa mchango wa maendeleo ya teknolojia katika utanzu wa hadithi za ngano. Hivyo utafiti huu ulijikita katika kuchunguza athari za maendeleo ya teknolojia katika ngano za Zanzibar.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

### 1.4.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza namna maendeleo ya teknolojia yanavyoathiri hadithi za ngano.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

a) Kuchunguza historia ya ngano katika jamii ya Wazanzibari.

b) Kuchambua maendeleo ya teknolojia ambayo yanaathiri ngano.

c) Kubainisha athari za maendeleo ya teknolojia katika hadithi za ngano.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

a) Je hadithi za ngano za Zanzibar zilikuwaje?

b) Ni maendeleo yapi ya teknolojia ambayo yameathiri hadithi za ngano?

c) Athari hizo zinajidhihirisha vipi katika uwasilishwaji, uhifadhi, usambazaji na dhima ya ngano?

## 1.5 Manufaa ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameleta manufaa yafuatayo: Yamesaidia kuwa ni hazina ya marejeleo kwa msomi wa fasihi simulizi, na kumpa fursa mtafiti mwengine atakayevutiwa na eneo hili kuweza kufanya utafiti kama huu kupitia tanzu nyengine za fasihi simulizi. Mtafiti amebaini kuwa teknolojia imepoteza vionjo vya asili ya kiutamaduni.

## 1.6 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo inabainisha kuwa sanaa inasawiri na kusawiriana na hali halisi ya jamii.Yaani fasihi ikiwa ni sanaa ambapo chimbuko ni katika jamii inajikita katika hoja kwamba kazi yeyote ya sanaa husawiri

hali halisi katika jamii pamoja na mabadiliko ambayo kwa kawaida huathiri kazi ya sanaa hiyo.

Nadharia hii inajikita katika fikra za Marx na Engels (Simiyu 2011: 24) ambao waasisi wake wanadai kuwa mwanadamu ni zao la maumbile asilia ya ulimwengu na kuwa mabadiliko ya mwanadamu kutoka hali ya unyama kuingia katika hali ya ubinadamu halikuwa jambo la siku moja, au wiki moja tu ila yamechukua mamilioni ya miaka.

Nadharia hii imefafanua kuwa mwanadamu alibadilika alipoanza kufanya kazi na kuzalisha mali na hivyo kukabiliana na mazingira ya kimaumbile aliyoyakuta katika uzalishaji huo wa mali. Mwanadamu kwa hivyo ilibidi ashirikiane na wenzake. Kwa sababu hiyo alihitaji chombo cha kuwasiliana na kuelewana nao. Lugha ilianza kama njia tu ya kurahisisha mawasiliano hayo. Baadaye lugha hiyo ikawa chomba cha sanaa ikiwemo fasihi. Kwa kadiri maendeleo ya uzalishaji yalivyoongezeka na kumpa mwanadamu muda wa ziada wa kujiburudisha na kujistarehesha kwa njia ya sanaa, fasihi ilianza kujitenga na kazi za uzalishaji, ikawa ni sanaa ya uburudishaji au ya shughuli maalumu za kijamii ikiwamo sherehe, ibada na kadhalika. Kwa muktadha huu, maendeleo ya teknolojia yaliyotokea katika jamii bila shaka yana athari kubwa kwa fasihi ya jamii ama chanya au hasi kwani fasihi ni zao la jamii na hivyo haiwezi kutengwa na uhalisi huo.

**Hitimisho**

Katika sura hii tumechunguza namna teknolojia inavyoathiri ngano katika mkoa wa Mjini Magharibi katika kisiwa cha Unguja. Pia tumeonesha utangulizi, usuli wa tatizo, tamko la utafiti, malengo ya utafiti (lengo kuu na malengo mahsusi), maswali ya utafiti ambayo yanahoji namna hadithi za ngano zilivyokuwa Zanzibar,

maendeleo yapi ya teknolojia yanayoathiri ngano pamoja na athari hizo zimejidhihirisha vipi katika utungaji, usambazaji, uhifsdhi na hata dhima.Pia manufaa ya utafiti yameainishwa. Manufaa hayo ni pamoja na kuwa imekuwa ni hazina ya marejeleo kwa wasomi wa fasihi simulizi na kumpa fursa mtafiti mwengine kweza kufanya utafiti kama huu kupitia tanzu nyengine. Na mwisho, sura hii imebainisha nadharia ambayo imeongoza utafiti huu. Nadharia hiyo ni ya uhalisia inayodai kuwa fasihi ni zao la jamii, hivyo haina budi kusawiri na kusawiriana na hali halisi ya jamii. Kwa hivyo fasihi hubadilika kwa kadri jamii inavyobadilika.

## SURA YA PILI

### 2.0 Utangulizi

Sehemu hii imebainisha picha ya jumla ya maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada hii. Maandiko hayo yamegawika katika sehemu kuu tatu. Kwanza ni maandiko kuhusu fasili ya teknolojia. Pili ni maandiko kuhusu maendeleo ya teknolojia na nafasi yake katika fasihi ya jamii, na tatu ni maandiko yanayohusu hadithi za mapokeo (ngano) na historia yake.

### 2.1 Maandiko kuhusu Teknolojia

### 2.2 Fasili ya Teknolojia

Fasili ya teknolojia kama inavyojidhihirisha katika ufafanuzi wa istilahi, inatubainishia wazi  mambo muhimu yanayohusu teknolojia. Mambo hayo ni kuwa teknolojia ni maarifa ya sayansi ambayo yanawekwa katika matumizi ya vitu kama vile zana au mitambo. Kwa kuzingatia dhana ya utafiti huu, tumeona kuwa hadithi za kimapokeo zimekumbwa na utumiaji wa teknolojia kama vile runinga, CD, radio na maandishi katika uwasilishwaji na uhifadhi wake kuliko ilivyozoeleka hapo nyuma ambapo njia ya kichwa na kutoa kwa mdomo vilizoeleka. Malengo ya teknolojia pamoja na mambo mengine ni kumuwezesha binadamu kuweza kukabiliana na mazingira yake kwa urahisi zaidi.

#### 2.2.1 Nafasi ya Teknolojia katika Fasihi

Utumiaji wa teknolojia huwa na manufaa chanya na hasi kwa binadamu ambao huonekana katika utendaji. Watoto waliozaliwa katika zama hizi ambao wangine huziita ni zama za sayansi na teknolojia wamepiga hatua kubwa ya maendeleo, ambao huwa wanakulia katika ulimwengu unaowanyima muda wa kukaa na wakubwa zao (wawe wazazi, mabibi, mababu/ dada zao) ili kusimuliwa hadithi.

Walio wengi hasa ni wale wanaoishi mijini na ambao hawaipati fursa ya kuifaidi fasihi simulizi katika dhana yake na umbo lake lile linalosisitiza kusambazwa kwa mdomo na kuhifadhiwa kichwani. Ingawa katika sehemu za vijijini bado watoto wanaipata fursa hiyo. Hata hivyo, kwa dunia inavyobadilika watoto hao wawe mashuleni, majumbani na hata ambao wamemaliza kiwango fulani cha elimu huwa wanaipata fasihi simulizi ya kijadi katika maana na umbo linaloendana na wakati wao. Kadiri dunia ibadilikavyo kwa upande wa sayansi na teknolojia, ndivyo na tanzu za fasihi simulizi zinavyobadilika au zinavyopaswa kubadilika kama Kezilahabi (1995) anavyoeleza anapozungumzia Fasihi ya Kiswahili:

> *Ieleweke kwamba fasihi ya Kiswahili imo katika karne ya*
>
> *Teknolojia lazima ijieleze katika mazingira hayo na kukua*
>
> *kwake hakuwezi kutenganishwa na teknolojia ya leo.*

Kutokana na nukuu hii utafiti huu umegundua kuwa hadithi za ngano za Zanzibar zimeathiriwa sana na usasa wa teknolojia. Miongoni mwa teknolojia ambayo hutumika kuhifadhia, kusambaza na kuwasilisha hadithi za kimapokeo ni pamoja na taeknolojia ya uchapishaji, unasaji sauti, intaneti, video na kadhalika. Vyombo hivi vinapotumika huleta athari kubwa kwa hadithi za ngano katika uwasilishaji, uhifadhi, usambazaji na hata dhima yake. Mutembei (2005:11) anaonesha athari hizo kwa kulinganisha hali ilivyokuwa hapo kale na ilivyo sasa. Anafafanua kuwa hapo kale uwasilishwaji wake ulifanywa kwa mdomo na msanii alikabiliana ana kwa ana na hadhira yake na pale anapokufa sanaa hiyo hukoma, maana sanaa hukaririwa kichwani. Usambazaji ulifanywa na msanii kwa mdomo wake na alikuwa na uhuru wa kubadili matini yake kulingana na matakwa yake na muktadha uliomkabili. Kwa

upande wa muktadha wa sayansi na teknolojia uwaasilishwaji hufanywa kwa mdomo, na pia vifaa kama vile redio, TV, video, kanda na kadhalika. Athari kadha wa kadha zimeonekana kutokana na maendeleo ya teknolojia kwenye fasihi simulizi kama vile nyimbo, uigizaji na nyenginezo. Mutembei (2005:11) anaainisha athari hizo kwa kulinganisha hali ilivyokuwa hapo kale na sasa kwa kutuonesha jadweli ifuatayo:

**Jadweli 1: Ulinganishaji wa fasihi simulizi wa kijadi na kisayansi**

| | KUTOLEWA KUWASILISHWA | KUHIFADHIWA | KUSAMBAZWA | MATINI YAKE |
|---|---|---|---|---|
| SASA | Mdomo, chombo kama vile Redio, TV, video kanda | Chombo kama Redio, TV, Video intaneti | Sauti ya msanii inapatikana katika vifaa | Inaweza isibadilike hasa ikihifadhiwa katika vifaa |
| KALE | Mdomo, msanii yupo. Akifa njia hii yam domo na kazi inakufa | Kichwani mwa msanii | Msanii mwenyewe kupitia mdomo wake | Inabadilika badilika |

**Chanzo**: Mutembi, (2005: 11)

Kutokana na jadweli hili tunaona kuwa uwasilishwaji wa fasihi simulizi, ngano ikiwa moja kati ya tanzu zake, hapo kale uwasilishwaji wake ulifanywa kwa mdomo. Msanii alikabiliana ana kwa ana na hadhira yake na akifa sanaa hiyo hukoma maana sanaa ilihifadhiwa kwa kukaririwa kichwani. Usambazwaji ulifanywa na msanii

kupitia mdomo wake na alikuwa na uhuru wa kubadili matini yake kulingana na matakwa yake na muktadha uliomkabili.

Katika muktadha wa maendeleo ya teknolojia, uwasilishwaji hufanywa kwa mdomo na pia kwa vyombo kama vile redio, T.V, video, kanda na kadhalika. Katika matumizi ya vifaa hivi si lazima msanii awepo kwa vile huwa imehifadhiwa kwenye vifaa kama kanda za redio kaseti, televisheni na intaneti ambazo husambazwa kupitia kwenye vifaa hivyo. Matumizi ya teknolojia hii yanamfanya msanii asiwe huru kubadili kazi yake hadi atakaporikodi kazi hiyo upya, lakini kazi hiyo inaweza kudumu kwa miaka mengi iwapo itahifadhiwa vizuri.

Wamitila (2003:6) anaizungumzia athari ya maendeleo ya teknolojia katika fasihi simulizi kwa kusema;

> *'Katika tamaduni andishi', ambazo zimeathiriwa na mfumo wa kimaandishi, hiyo inayojulikana kama fasihi simulizi sio simulizi tena bali inahifadhiwa kwa njia mbalimbali kama vile vinasa sauti, kanda za video na kompiyuta.*

Aidha Khamis (1983:3) anaeleza kuwa fasihi simulizi imevizwa kwa maendeleo ya kiufundi na uvumbuzi wa mashine kadhaa hasa za uchapaji na za mawasiliano zikiwemo redio, tepurikoda na televisheni. Kutokana na mitazamo hii tunaona kuwa maendeleo ya teknolojia yana athari kubwa kwa hadithi za ngano.

### 2.2.2 Maandiko Kuhusu Maana na Sifa za Hadithi za Kimapokeo

Hadithi za kimapokeo ni hadithi za jadi ambazo huwasilishwa kwa njia ya mdomo. Hadithi hizi zinasimuliwa na kutambwa mbele ya hadhira. Sifa za hadithi hizi

zimeelezwa na Simiyu (2011) ambapo anaeleza kuwa hadithi huwa na mwanzo na miisho maalumu.

Hadithi za mapokeo mara nyingi huanza na maneno ‘paukwa- pakawa’ au ‘hadithi-hadithi’, na kutumia lugha ya kimaelezo. Hii ina maana kuwa hadithi zipo katika lugha ya kinathari zikiwa katika mtindo wa moja kwa moja kueleza tukio au matukio. Hadithi husheheni wahusika wanyama, watu, mazimwi au vitu mbalimbali. Wahusika hawa hubebeshwa uhusika ambao unaakisi matendo ya binadamu Vilevile hutumia tanzu nyegine za fasihi simulizi kama vile nyimbo, methali misemo na tamathali za semi kwa dhamira mbalimbali. Kwa mfano hutumia mbinu hizi kwa ajili ya kuburudisha, kuamsha hadhira, kutoa mafunzo, kupamba lugha na kufikisha ujumbe. Aidha hadithi hizi huwa na tukio moja kuu na matukio mengine madogo madogo. Kwa upande wa mtambaji wa hadithi huwa na sifa zifuatavyo; fanani lazima awe mahiri wa lugha ili atongoe hadithi bila ya kusitisita, washirikishe hadhira, awe mcheshi, awe na uwezo wa kuingiza baadhi ya mambo kwa kutumia ishara, kutofautisha sauti, matumizi ya maleba, kubadilisha matendo na miondoko.

### 2.2.3 Historia ya Hadithi za Kimapokeo

Kila jamii ina aina zake za hadithi za kimapokeo. Hadithi hizo hutolewa katika nyakati maalum. Mara nyingi hutolewa wakati wa jioni kwa ajili ya kuwaburudisha watu. Katika jamii ya Zanzibar hadithi zilitolewa wakati wa jioni. Wazee ndiyo ambao walibeba jukumu la kutamba hadithi hizo. Wakati wa jioni ndiyo ulikuwa muafaka kwa sababu mbili kuu; ni wakati wa kusubiria chakula (chajio) kwa lengo kuwafanya watoto wasilale kwani chajio kilikuwa kinapikwa jioni na pili ni wakati wa kuchambua karafuu, hasa huko Pemba ambako zao hili huvunwa. Lengo lake

hilo kwa watu wazima ni kuwashajiisha watu kufanya kazi hiyo bila ya kujisikia na uchovu.

Kwa kawaida, hadithi zilitambwa kufungamana na muktadha fulani wa kijamii. Hadithi zilihifadhiwa kichwani na kusambazwa kwa mdomo kama ilivyoelezwa hapo kabla. Mtambaji alikuwa akibadilika kulingana na muktadha na pia hadhira yake na huwepo uso kwa uso, hivyo alishiriki kikamilifu katika matendo kama vile kuimba, kuuliza maswali, kuitikia na kadhalika. Pia Mulokozi (1996) anasisitiza kuwa wasikilizaji ndiyo ambao hushiriki na kuhakiki sanaa inayowasilishwa na fanani. Hadithi za kimapokeo ziliendelea kutambwa hata baada ya ujilio wa wageni pamoja na wakoloni. Wakati wa ukoloni ambapo wakaazi wa visiwa hivi walipata fursa ya kusoma na kuandika, hasa baada ya mashirika ya uchapishaji kuzuka na kuchapisha vitabu vya Kiswahili. Hadithi zilikusanywa na kuandikwa kwa lengo la kuibua na kukuza vipaji vya wasanii na kuitangaza fasihi ya jamii hizo. Mashindano ya uandishi wa hadithi nayo yalifanywa. Hali hii iliendelea hata baada ya uhuru ambapo shirika la *East African Publishing House* lilipoona kwamba kuna upungufu wa waandishi na kazi za fasihi na hivyo lilitangaza mashindani ya uandishi wa hadithi na kuzichapisha mnamo mwaka 1965 (Rajmond, O 1991: 1).

### 2.2.4 Pengo la Utafiti

Kwa jumla kazi za wataalamu wote hawa zimejadili juu ya mambo yanayohusiana na hadithi za kimapokeo. Mambo hayo yanakidhi haja kutokana na mikabala na miegamo yao waliyodhamiria. Hata hivyo bado kuna mapengo kadhaa kuhusiana na hadithi za kimapokeo kwa upande wa hadithi za ngano. Kimoja wapo ni kuwa hakuna vitabu wala majarida yanayoonesha kuwa maendeleo ya teknolojia

yanaathiri hadithi za kijadi za ngano katika uwasilishaji, usambazaji, uhifadhi na dhima. Kwa hivyo, utafiti huu unakusudia kuziba pengo hilo.

### 2.2.5 Hitimisho

Katika sura hii maandiko mbalimbali yanayoelezea maana ya teknolojia na nafasi yake katika fasihi ya jamii yameangaliwa. Aidha maandiko yanayohusiana na maana na sifa za hadithi za ngano yameangaliwa na kumalizia kwa pengo la utafiti ambalo lipo na lazima lizibwe.

# SURA YA TATU

# USANIFU NA MBINU ZA KUKUSANYIA DATA

## 3.0 Utangulizi

Sura ya tatu imefafanua mpango wa jumla wa utafiti huu, mbinu za kukusanyia data, zana na vifaa vya utafiti, jamii ya watafitiwa, eneo la utafuti mchakato mzima wa ukusanyaji na uchambuzi wa data na uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti.

## 3.1 Mpango wa Utafiti

## 3.2 Mkabala wa uchambuzi wa data

Utafiti huu ni wa kitaamuli: hivyo haukuhusisha taarifa za kitakwimu. Mkabala huu ulitumika kuchambua data kutoka kwa wahojiwa mbalimbali na baadaye mtafiti kuhakiki maelezo yao. Tafiti za kitaamuli hutumia mbinu za maelezo, ulinganishi wa data dhidi ya nadharia katika kuchanganua data zake na kutoa matokeo Ponera (2013) akimnukuu Baradyana na Ame, (2007:65) alieleza. Hivyo basi, ukusanyaji, uchanganuzi wa data, pamoja na utoaji wa matokeo ya utafiti huu uliegemezwa katika mbinu hii. Sehemu kubwa ya data za utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Data zilikusanywa kupitia maandiko mbalimbali yaliyokusanya hadithi za kimapokeo za ngano za Zanzibar. Aidha data za uwandani zilipatikana kupitia mijadala ya vikundi, na mahojiano ya ana kwa ana. Data mbalimbali zilikusanywa, kuhakikiwa, kuchanganuliwa, na hatimaye kufafanuliwa kwa kina.

## 3.3 Walengwa wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kushirikisha makundi makuu matatu ambayo yalikuwa ndiyo chanzo cha kukusanyia taarifa za utafiti katika ujumla wake na sampuli ilichaguliwa.

### 3.3.1 Makundi tafitiwa

### 3.3.2 Waalimu wa SUZA

Walimu wa SUZA ambapo awali wakijulika kama TAKILUKI wao wanajishughulisha na ukusanyaji na uandishi wa kazi za fasihi simulizi, ngano ikiwa ni miongoni mwa kazi hizo. Hivyo walimu hao wameweza kusaidia kubainisha baadhi ya hadithi za ngano walizokusanya katika mkoa wa Mjini Magharibi. Vile vile wametoa maelezo juu ya historia na njia za kiteknolojia zinazotumika kuwasilishia, kuhifadhia na kusambazia ngano Zanzibar.

### 3.3.3 Wafanyakazi wa ZBC

Watafitiwa wa ZBC hawa ni wafanya kazi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar. Wao walisadia kutoa taarifa juu ya namna wanavyopita maskulini na kurikodi vipindi, njia wanazotumia katika kuhifadhia ngano wanazozikusanya pamoja kubainisha athari ambazo hupatikana inapotumika teknolojia ya sasa kuziwasilisha, kuzisambaza na kuzihifadhi ngano kupitia vifaa hivyo.

### 3.3.4 Wanafunzi wa Sekondari

Wanafunzi wa sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne ambao walijadili kupitia vikundi athari zinazopatikana kutokana na utumiaji wa vifaa vya teknolojia vya kisasa kama vile televisheni, kompyuta, intaneti, CD na kadhalika katika hadithi za ngano; hayo yalijitokeza katika uwasilishaji, usambazaji, uhifadhi na dhima.

### 3.3.4 Wakazi wa Zanzibar

Wakaazi wa Zanzibar katika mkoa wa Mjini Magharibi nao walihusishwa katika utafiti. Watu hawa wamesaidia kutoa taarifa ambazo zimesaidia kujibu maswali ya utafiti. Wakaazi waliohojiwa wamepatikana katika maeneo ya Mwanyanya na Mtoni. Wao walisaidia kueleza historia ya hadithi hizi pamoja na mifano ya hadithi

hizo na pia kutoa taarifa juu ya vipindi vya redio na televisheni vinavyoonesha vipindi vya watoto ambamo ngano husimuliwa. Wakaazi hawa walipatikana kwa msaada wa sheha.

### 3.4 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli ya watafitiwa ilipatikana kwa kutumia sampuli lengwa. Hii ni mbinu ya usampulishaji ambayo humruhusu mtafiti kuwachagua wawakilishi kulingana na jinsi watakavyokidhi haja na malengo ya utafiti. Kwa mujibu wa Kothari (2009) sampuli nzuri ni ile iliyo ndogo, jumui na itakayomwezesha mtafiti kuidhibiti. Kwa hivyo, utafiti huu umefuata kigezo hiki katika uteuzi wa sampuli. Kwa hivyo utafutaji wa wa sampuli umehusisha watafitiwa 38 kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi: kati ya hao wawili ni wazee kutoka katika shehia mbili tofauti kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi. Walimu wawili kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzbar (SUZA), wanafunzi wa sekondari 15 kuanzia kidato cha 1- 4 kutoka katika skuli mbili zilizomo katika wilaya mbili za mkao wa Mjini wa Magharibi. Wazee wamehojiwa juu ya uwepo wa usimuliaji wa hadithi za kimapokeo katika sehemu zao na kama kuna athari yeyote ambayo imejitokeza kutokana na ujio wa sayansi na teknolojia kwa hadithi hizo. Kwa upande wa wanafunzi wamefanya mjadala wa vikundi juu ya athari ambazo zinapatikana kutokana na utumiaji wa vifaa vya teknolojia katika utungaji, uwasilishwaji, uhifadhi, usambazaji, na dhima za hadithi za ngano. Na wafanyakazi wawili wa Shirika la Utangazaji Zanzibar ambao wanajishughulisha na kurikodi hadithi za ngano katika skuli mbalimbali kwa kutumia teknolojia ya kama vile tepurikoda na CD.

### 3.4.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika maeneo mawili makuu ambayo ni maktabani na uwandani. Utafiti wa kimaktabani umefanyika katika maktaba za SUZA, BAKIZA na ZBC ambazo zinapatikana Zanzibar. Hii ni kwa sababu maktaba hizi zina wingi wa vitabu na makavazi yanayohusiana na mada. Kwa upande wa uwandani, utafiti umefanyika katika maeneo ya Mwanyanya na Mtoni. Maeneo haya yamechaguliwa kutokana na ukaribu wa makazi ya mtafiti na kwa kiasi kikubwa bado hayajaathiriwa sana na teknolojia za kisasa, hivyo mtafiti ameweza kupata taarifa ambazo zimeweza kutosheleza utafiti huu. Maskuli ambayo utafiti huu umefanyika kutoka kwa wanafunzi wa sekondari iliyopo Mfenesini ambayo ipo ng'ambo ya mji na skuli ya Benbella ambayo ipo mjini. Skuli hizi zimeteuliwa kwa sababu ni skuli za sekondari ambamo somo la Fasihi Simulizi linafundishwa.

## 3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii yenye kuhusisha mbinu za ukusanyaji wa data inaeleza mbinu, njia na zana mbalimbali zilizotumika katika mchakato mzima wa ukusanyaji data.

### 3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Njia kuu za kukusanyia data za utafiti huu zilizotumika ni za udurusu wa kimaktaba, mahojiano na mjadala wa vikundi. Zana ambazo zimetumumika ni pamoja na mwuongozo wa udurusu na usaili pamoja na kifaa cha kunasia sauti. Aidha kalamu na karatasi za kuandika dondoo zinazotolewa na wahojiwa.

### 3.5.2 Udurusu wa Kimaktaba

Katika utafiti huu, mtafiti alitembelea katika maktaba za BAKIZA, SUZA, na ZBC. Aidha mtafiti alisoma vitabu mbalimbali ili kupata data (taarifa) muhimu juu ya mada anayoitafiti.

### 3.5.3 Usikilizaji wa vyombo vya Habari

Mtafiti wa kazi hii pia alisikiliza vipindi vya watoto kupitia redio na pia kutazama televisheni. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuchungua namna hadithi, ambazo ndizo anazozifanyia utafiti, zinavyowasilishwa na kusambazwa.

### 3.5.4 Mahojiano

Kothari (2009: 97) anasema kuwa mahojiano au usaili ni mpangilio mzima wa maswali yenye lengo la kutafuta data au taarifa kwa njia ya mazungumzo ya ana kwa ana. Katika utafiti huu mtafiti alifanya mahojiano ya ana kwa ana na wakaazi wa mkoa wa Mjini Magharibi, walimu wa SUZA, na wafanya kazi wa ZBC. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata taarifa muhimu zinazohusiana na mada anayoitafiti.

## 3.6 Vifaa na zana za kukusanyia data

### 3.6.1 Kalamu, penseli na karatasi

Mtafiti alitumia kalamu na karatasi katika kukusanya data. Wakati wa mjadala wa vikundi vifaa hivi vilitumika kuandika mawazo ya wanafunzi juu ya mada ikiwa ni data ambazo zimechambuliwa. Vile vile vifaa hivi vimetumika kuandikia taarifa (data) za wahojiwa. Vifaa hivi ni vya kawaida, vilipatikana, havina gharama kubwa na vilitumika.

### 3.6.2 Simu ya Mkononi

Kifaa hiki kilitumika kurikodia sauti ili kuweka kumbukumbu na hivyo mtafiti kuweza kuzitumia taarifa zilizorikodiwa katika uchambuzi wa data. Pia kifaa hiki kilitumika kuwasiliana na watafitiwa kadha pamoja na msimamizi wa kazi hii.

### 3.6.3 Redio na Televisheni

Vifaa vya redio na televisheni vilitumika kusikilizia na kuangalia vipindi vya watoto vinavyorushwa hewani. Katika vipindi hivyo watoto huwa na kazi mbalimbali za

fasihi simulizi pamoja na hadithi ikiwa ni miongoni mwa kazi hizo. Mtafiti alirikodi taarifa ambazo zinahusiana na mada yake.

### 3.6.4 Kompyuta

Kompyuta imetumiwa kuchapia kazi, kuzichambua data pamoja na kumtumia msimamizi kwa kuziangalia kwa ajili ya marekebisho. Aidha mtafita ametumia kompyuta kutafuta data zinazohusiana na mada katika mtandao.

## 3.7 Ukusanyaji wa Data na Udhibiti

Maadili yaliyoongoza utafiti huu yamezingatiwa kadiri ilivyowezekana. Mambo muhimu ya kupata ridhaa ya wahojiwa, kulinda na kuhifadhi taarifa za siri na kuhifadhi majina ya wahojiwa kadiri ya walivyotaka yalifanyiwa kazi. Data za maktabani zimekusanywa kwa njia ya kudurusu kwa kuzingatia mwongozo wa udurusu. Data hizo zimekusanywa kwa njia ya mjadala wa vikundi na mahojiano ya ana kwa ana. Mwongozo wa usaili umetumika kuwahoji wakaazi wa shehia zilizotajwa pamoja na watangazaji wa ZBC. Wanafunzi walifanya majadiliano ya vikundi kutokana na mwongozo ambao walipewa na mtafiti. Mtafiti amesaidiwa na walimu waliwaongoza wanafunzi kufanya majadiliano katika vikundi vyao juu ya mada husika.

### 3.7.1 Mipaka ya utafiti

Mipaka ya Utafiti huu umelenga kubainisha na kuchambua athari za maendeleo ya teknolojia katika hadithi za ngano; mifano hadithi za ngano zilitoka katika jamii ya Wazanzibari wanaoishi katika mkoa wa Mjini Magharibi. Aidha utafiti huu unaeleza athari hizo zinavyojitokeza katika uwasilishaji, usambazaji, uhifadhi na dhima. Fani na maudhui katika hadithi hizo havikushughulikiwa.

### 3.7.2 Vikwazo vya Utafiti

Mtafiti wa utafiti huu alipata vikwazo vifuatavyo katika mchakato mzima wa utafiti:

#### 3.7.2.1 Uelewa Mdogo wa Dhana ya Ngano

Kutokana na kuwa kwa wakati tulionao, hasa sehemu za mjini, ngano ni kitu kigeni ndani ya masikio ya walio wengi, mtafiti ilimchukua muda kupata watu ambao wanaielewa dhana hii. Wakaazi wengi ambao wamezaliwa na kukulia katika mkoa wa mjini Magharibi si rahisi kuzielewa ngano hizo. Watu ambao walikuja kupatikana ni wahamiaji kutoka sehemu za vijijini Unguja na kisiwani Pemba ambao wameshaishi kwa muda mrefu katika mkoa huu. Hivyo upatikanaji wa watu hawa kulifanikiwa kwa msaada wa masheha na wenyeji waliomo katika maeneo yaliyoteuliwa.

#### 3.7.2.2 Urasimu katika Kupata taarifa katika Vyombo vya Habari

Moja katika tatizo ambalo lilimkabili mtafiti ni kule kupata taarifa katika vyombo vya habari alivyoviteua kwa wakati. Kulikuwa na urasimu mkubwa aliopambana nao mtafiti licha ya kuwa alishapata kibali kutoka serikalini. Mtafiti alitakiwa kupatiwa uthibitisho wa barua kutoka kwa katibu Mkuu wa *Wizara ya Habari na Utamaduni*. Barua ilipatikana, hata hivyo, Mkurugenzi wa ZBC alimtaka mtafiti kuandika barua nyengine itakayoainisha utafiti huo ungefanywa katika maeneo gani. Jambo hili lilichukua muda. Hatimaye mtafiti aliwasilisha barua hizi na kuruhusiwa kukusanya data.

#### 3.7.2.3 Upungufu wa Fedha

Utafiti huu ulifanyika huku mtafiti akiwa na upungufu wa fedha za kukamilisha mchakato huu. Ingawa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar iliahidi kudhamini, fedha ambazo mtafiti alipatiwa hazikuweza kukidhi haja katika

kukamilisha mchakato wote. Kama inavyoeleweka kuwa utafiti unahitaji fedha nyingi, mtafiti ilimbidi kupatiwa baadhi ya fedha na wanafamilia.

#### 3.7.2.4 Ukosefu wa Vitabu

Hali ya ukosefu wa baadhi yavitabu imetokana na kutokuwepo kwa baadhi ya vitabu katika maktaba ambazo mtafiti aliziteuwa kufanya utafiti. Hivyo kulimkosesha kabisa baadhi ya nakala muhimu zinazohusiana na mada. Mtafiti ilimlazimu kwenda Nyumba ya Nyaraka baada ya kushauriwa na msimamizi wake ambako alizipata baadhi na nyengine kukosekana kabisa. Moja kati ya nakala iliyokosekana ni *Paukwa za Zanzibar*

**Hitimisho**

Katika sura hii tumejadili usanifu na mbinu za utafiti kwa jumla. Mpango wa utafiti, walengwa wa utafiti, usampulishaji na sampuli, eneo la utafiti, njia za kukusanyia data, zana na vifaa vya kukusanyia data pamoja na mipaka ya utafiti na kuishia na vikwazo vya utafa

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, data zillizokusanywa zimewasilishwa na kuchanganuliwa ili kujibu maswali ya utafiti. Uwasilishaji umegawanyika katika sehemu kuu tatu ili kuakisi malengo ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza imechunguza kwa muhtasari historia ya Fasihi katika jamii ya Zanzibar kwa kuangalia asili na chimbuko lake. Baadaye imechunguza asili na chimbuko la ngano kwa kuzingatia utungaji, uwasilishaji, uhifadhi, usambazaji na dhima yenyewe. Sehemu ya pili imebainisha teknolojia inayotumika Zanzibar kwa kuwasilisha, kuhifadhia, na kusambazia hadithi za ngano. Sehemu ya tatu imetathmini athari chanya na hasi zinazotokana na utumiaji wa teknolojia katika utungaji, uwasilishaji, uhifadhi, usambazaji na dhima za ngano. Ngano saba teule kutoka kwa wanajamii na maandiko yaliyopitiwa zimechukuliwa na kutumiwa katika mjadala huu kutolea mifano katika kufafanua hoja mbalimbali. Ngano hizo ni hadithi ya *Jongoo na Nyoka* ambayo ni kisasili, hadithi ya *Mnara wa Baba na Mama*, hadithi ya *Mtendazema*, hadithi ya *Zimwi*, hadithi ya *Sungura na buyu la asali,* hadithi ya *Kinyonga Mfalme wa Wanyama* na hadithi ya *Mcheka Kilema.*

## 4.1 Historia ya Fasihi katika Jamii ya Zanzibar

Kila jamii ina sanaa zake ambazo huzitumia kuwasilisha hisia zao za ndani ambazo ni miongani mwa sanaa hizo ni fasihi. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa ufundi ili kuwasilisha hisia za ndani za mwanadamu. Jamii ya Wazanzibar ni jamii ya watu ambao wana mila, tamaduni na silka zao. Utafiti huu umebaini kuwa jamii hii ilikuwa na shughuli ambazo ziliwalazimu watu kutumia kazi za fasihi. Fasihi ya Kiswahili ya Zanzibar inaonekana kuwa imeathariwa kwa kiasi fulani na Uarabu na

Uislamu ndani yake. Fasihi ambayo ilitumika kama ilivyo kwa jamii za Kiafrika, ilikuwa ni fasihi simulizi kwani wenyeji hawakujua kusoma wala kuandika. Miongoni mwa tanzu za fasihi zilizotumika ni pamoja na nyimbo, ngoma, utani, vitendawili na hadithi. Katika shughuli kama za harusi, unyago, uvuvi na pungo na nyenginezo walitumia kazi za sanaa kuelekezana, kufunzana na kufarijiana. Hali hii inaendelea hadi sasa kwa baadhi ya maeneo ya vijijini. Vikundi vya sanaa kama vile taarabu, michezo ya kuigiza na kadhalika, vinaendelea kufanya kaz ya kazi ya kifasihi kama Khamis na wenzake (2008:17) wanavyoeleza:

> *Ama kwa upande wa usanii wa lugha,*
> *Waswahili wana tungo zao za nyimbo,*
> *mashairi, tenzi na nganjera za aina mbali*
> *mbali*

Khamis na wenzake (2008) akiendelea katika makala yake, anafafanua kuwa Waswahili ni watu wenye fasihi yao ambayo haipaswi kudharauliwa na kubezwa. Kwani kupitia sanaa hii ndiyo tamaduni, amali na silka zao zinamofafanuliwa. Anafafanua kuwa Fasihi Simulizi imekuwa ikitumika katika shughulli mbali mbali za kijamii kabla ya kuibuka kwa maandishi katika jamii hizo. Kutokana na ufafanuzi huu, utafiti umebaini kuwa fasihi ya watu wa jamii ya Wazanzibar ni Fasihi Simulizi kwa asili yake na chimbuko lake linatokana na kazi na shughuli za kijamii. Kazi hizi ziliwasukuma kubuni sanaa ya lugha ambayo ingewaliwaza na kuwaburudisha kutokana na uchovu wa kazi. Aidha kwa kutumia sanaa hii, walirekebishana, walifundishana, waliasana na kunasihiana juu ya tabia na hulka zinazokubalika katika jamii yao.

Pamoja na kuwa fasihi ya watu wa visiwa hivi ni ya Kiswahili, utafiti huu umebaini kuwa imo athari kubwa za fasihi ya kigeni hasa Waarabu. Kama ilivyo kawaida,

maingiliano ya watu wa jamii tofauti husababisha kuathiriana kiutamaduni, ndivyo ilivyo kwa jamii ya Waswahili wa Zanzibar. Kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa Zanzibar ni jamii yenye mwingiliano mkubwa na watu wa jamii nyengine, na pia utamaduni wake ni changamani. Basi hata fasihi yake imepata athari hizo. Kwa mfano jamii ya Waarabu walileta *Taarabu* na hadithi za *Alifu U Lela U Lela*, hadithi za *Abunuasi*, *Maulidi ya Homu* na kadhalika. Wahojiwa wengi walidai kuwa Waarabu na koo zao walikuwa wanapenda sterehe, hivyo walikuwa wakitenga muda wa kusikiliza taarabu na kusimuliana hadithi. Utamaduni huu baadaye ukasambaa na Waswahili wakauigiza katika tamaduni zao. Taarabu ni ngoma ambayo inapendwa Zanzibar. Mbali na hayo Waarabu walichanganya damu na Waswahili kwa njia ya ndoa hivyo utamaduni wao nao uliingiliana na ule wa Waswahili, kama Khamis (1983:6) anavyoeleza :

> *Uchunguzi wangu wa ghafla unaonesha amali*
> *za Kiarabu katika tanzu kadhaa za fasihi simulizi;*
> *kwa mfano, methali na vitendawili; mbali na*
> *hadithi za mapokeo za akina Abunuasi na Alfu*
> *Lela U Lela. Hapa hatutaisahau ngoma ya*
> *taarabu; ngoma ambayo bila shaka yeyote ina*
> *asili ya kiarabu.*

Fasihi simulizi katika jamii ya Zanzibar inaendelea kukua na kuchukua nafasi kubwa katika jamii. Hata baada ya kuzuka kwa maandishi, bado fasihi hii inaendelea katika miundo mbali mbali. Sherehe za kitaifa nazo huitumia sanaa hii kutoa ujumbe kwa wananchi. Kuna vikundi mbali mbali kama vile vikundi vya ngoma vya *Jeshi la Kujenga Uchumi*, *Magereza* na *Jeshi la Wananchi*. Pamoja na hayo kuna vyombo

kama redio na televisheni ambayo hurusha hewani vipindi mbalimbali kuhusiana na ngonjera, mashairi, taarabu, hadithi, nyimbo methali na vitendawili.

Imeonekana kuwa chimbuko la Fasihi ya Zanzibar ni Fasihi Simulizi ambayo inatokana na wao wenyewe watu wa Zanzibar licha ya kuwa imeathiriwa sana na fasihi za kigeni hasa za Waarabu ambao walifanya maskani yao na kuoana na walichanganya damu. Ama kwa upande wa asili ya fasihi simulizi ya jamii hii zatokana na amali zilizokuwamo katika jamii yao kama vile ukulima, uvuvu, ukwezi, useremala na kadhalika. Shughuli za kijamii kama vile arusi, maulidi ya kuzaliwa Mtume (S.A.W), unyago na maadhimisho ya siku za kitaifa na fasihi simulizi hutumika.

### 4.2 Chimbuko na Asili ya Hadithi za ngao za Zanzibar

Ngano ni moja kati ya tanzu za fasihi simulizi ambazo Wazanzibari wanatamba nazo. Utafiti huu umebaini kuwa asili ya hadithi hizi kwanza, ni kuwatisha watoto juu kuacha tabia fulani isiyokubalika pamoja na kuwaadilisha baada ya kuwaona watoto wanakwenda mwendo usiofaa. Mmoja kati ya wahojiwa; Bi Sharifa Issa wa Mtoni mwenye umri unaokisiwa kufikia miaka themanini anasema,

> *Watoto tunawatolea hadithi tunapoona kosa*
> *ili kuwaogopesha na kuwatisha juu ya tabia mbaya*
> *walizonazo.*

Kwa maana hiyo ngano ilikuja kama ni chuo cha kutolea taaluma kwa watoto. Watoto ambao walikuwa wakitolewa ngano ni watoto wenye umri kati ya miaka saba hadi kumi na sita. Hii ni jamii ambayo ililelewa na kujengwa katika maadili ambayo jamii iliyakubali. Ngano hizo ziliendelea kutambwa kwa vizazi na vizazi hadi muda huu wa sasa.

Pili, kuna wanaodai asili ya ngano ni kuionesha jamii kuwa kuna baadhi ya watu wana uelewa wa mazingira yao. Kwa kuwa jamii imezungukwa na mazingira tofauti yakiwamo ya bahari, nchi kavu, misitu na anga; baadhi ya watu kutaka kujionesha ni kwa kiasi gani wanayaelewa mazingira hayo, walibuni ngano ambazo mazingira hayo yangejifafanua. Kwa mfano katika jamii ya Zanzibar kuna ngano zinazoonesha maisha ya wanyama msituni. Kuna ngano zinazoonesha mazingira ya mume mwenye mke zaidi ya mmoja au mtoto anayelelewa na mama wa kambo na mazingira yake, na ngano zinazoonesha mazingira ya baharini na kadhalika. Kwa mfano katika Fasihi Simulizi Zanzibar (1983: 84) kuna ngano inayoonesha mazingira ya bahari hasa wakati wa usiku. Mwandishi anaonesha kuwa kwenye bahari usiku kunakuwa na mazingira yasiyokuwa ya kawaida. Kwa mfano katika bahari kunaonekana nyumba kitu ambacho kwa mazingira ya Zanzibar si rahisi. Hadithi inatuonesha mazingira hayo kama ifuatavyo:

> *siku moja Rajab aliondoka usiku kama kawaida yake na kwa bahati mbaya ulivuma upepo mkubwa hata wavuvi wakapoteana kabisa. Rajab alijiona peke yake anakwenda, upepo ulimchukua hata mwisho akaona mbele yake kwa mbali sana, ipo nyumba kubwa sana yenye kung'aa mataa tokea chini mpaka juu. Rajab aliufuata mwangaza huo wa taa, hata akafika karibu na ile nyumba, akatupa nanga akashuka bila kuogopa chochote.*
>
> **Chanzo:** *Fasihi Simulizi Zanzibar* (1983: 84)

Tatu, baadhi ya wahojiwa wamedai kuwa ngano asili yake ni watu ambao walikuwa na uwezo mkubwa wa kutumia lugha kutaka kuonesha uwezo wao. Kupitia utanzu huu watu waliweza kuonesha vipawa na uwezo walionao katika utumiaji wa lugha.

Hivyo walibuni visa ambavyo waliifinyaga lugha na kuwavuta watu kuwasikiliza. Katika ngano hizo misemo, methali, tamathali za semi, nyimbo na nahau zilitumika; Ngano ya *Mnara wa Baba na Mama* katumia tamathali za semi za tashhisi zifuatazo;

*Mnara ulisogea hadi kumfikia Yule mtoto*

*Ndege aliimba: Nile mtama nisile!*

Chimbuko la hadithi ni kutokana na kuwa watu wa jamii za kale walipovumbua vifaa vya kutendea kazi vilivyo bora zaidi, walipata muda mwingi wa kupumzika na hivyo kubuni ngano ambazo zingewafariji zaidi. Naye Songoyi (1997:23) anafafanua kuwa hadithi za ngano zilichipuka katika kipindi cha mfumo wa utumwa ambapo kulikuwa na matabaka kati ya mabwana na watumwa. Ngano hizo zilitambwa wakati wa usiku hasa wakati wa mbalamwezi. Watoto walisimuliwa ngano wakiwa wameketi kando kando ya moto. Ngano zilisimuliwa usiku kwa sababu wasimuliaji wa hadithi husema kwa kuwatisha watoto kuwa, "*Mtu akitamba hadithi mchana, huota mkia.*" Kwa mujibu wa wahojiwa walisema kuwa maana ya msemo huu ni kuwa mchana ni wakati wa kazi. Watoto nao wanakwenda madrasa na skuli; hivyo kukaa na kutoa hadithi mchana kungeandaa taifa la watu wavivu. Wazee na wakubwa ndiyo ambao waliochukua jukumu la kuzitamba hadithi hizo. Hadithi ziliwaleta watoto karibu ikiwa ni moja kati ya utamaduni wa Wazanzibari kuishi kama ndugu kwa kusaidiana kwenye raha na shida. Vile vile baadhi ya wahojiwa wamesema kuwa ngano zilisimuliwa usiku kwa lengo la kupoteza muda baada ya kula chajio. Watoto walifanyiwa hivyo kusudi ili wasilale mapema na shibe.

Ngano za wakati huo zilibuniwa zikiwa na wahusika ambao waliwakilisha tabia za watu katika jamii. Kuna ngano ambazo zilitumia wahusika wanyama kama vile sungura, fisi, jongoo, chura, nyoka na mbwa. Hawa ni wanyama ambao

wanapatikana katika jamii ya Zanzibar. Pia kuna ngano ambazo zinazotumia wahusika binadamu, mazimwi na majini. Kwa vile fasihi ya Zanzibar imeathiriwa na Waarabu kama ilivyoelezwa hapo awali, ngano zao pia zina utamaduni wa kiarabu. Kuna ngano ambazo wahusika wake ni masultani na malkia; hawa ni watawala waliopo bara Arabu. Pia katika ngano hizo kuna athari ya dini ya Kiislamu kama vile kusali na imani nyenginezo. Vile vile hadithi hizi zilitambwa kulingana na muktadha na mahitaji ya wanajamii. Kwa mfano, hadithi inaweza kutambwa kuonesha ubaya wa choyo katika muktadha fulani na katika muktadha mwengine kutumika kuonesha ubaya wa kutokufanya kazi. Na hapa Waswahili wanasema *Hadithi ni ncha saba*. Katika jamii hii, kuna ngano nyingi zinazohusu ubaya wa mama wa kambo. Ngano hizi zinaonesha kuwa ni kawaida katika jamii ya Waswahili mwanamume kuwa na mke zaidi ya mmoja, kwa hivyo ngano hizo zimekuja kuwaonya wanaume hao wawe makini wanapooa mke zaidi ya mmoja. Kwa mfano katika ngano ya *Mnara wa Baba na Mama* mtoto anapata mateso ya mama wa baada ya kufariki mama yake. Mateso anayoyapata ni pamoja na kunyimwa chakula, kunyanyaswa, kunyang'anywa vyake pamoja na kufanyiwa hila za kudhulumiwa ni mama yake wa kambo na ndugu yake wa baba mmoja.

Iko mianzio maalum ya ngano Zanzibar, kama vile *Paukwa- Pakawa* au *Hadithi-hadithi, hadithi njoo*. Mianzio hii ni ya kifomula kama ilivyo kawaida kwa fasihi simulizi. Mianzio hii ipo kwa sababu ya kuifanya hadhira kuwa makini na kujiweka tayari kwa kile kinachotaka kuwasilishwa. Baada ya hadhira kuitikia na kukaa sawa, fanani huanza kusimulia ngano yake.

Katika jamii ya Wazanzibar kuna aina mbali mbali za ngano, ngano hizi zimegaiwa kutokana na wahusika waliomo katika ngano hiyo, au matendo ya wahusika na vile

vile masaibu yanayowakuta wahusika. Mgao huu umeelezwa na Wamitila (2003), lakini zikichunguzwa ngano za Zanzibar nazo zinaingi katika makundi hayo. Makundi ya ngano hizo ni haya yafuatayo:

**i) Ngano za Ayari**

Hizi ni ngano ambazo muhusika mmoja mjanja anawashinda wegine kutoka katika matatizo fulani kwa kutumia ujanja. Aina hii ya ngano kwa Zanzibar inawakilishwa na ngano za Abunuasi, sungura au kinyonga; Mfano hadithi ya Kinyonga, katika ngano hii kinyonga amepata ushindi kutokana na ujanja wake. Laiti kama kinyonga hakujifunga katika mkia wa paa angefika mwisho na kwa hiyo angekosa ufalme. Kwa hivi ngano hii ni aina ya ngano ya ayari kwa vile kinyonga alivyofanya ni ujanja na kupata ufalme. Haditi inasema:

> *Kinyonga alijikongoja akichapia matawi ya miti kuelekea kwenye kiti Kadiri alivyojitahidi hakuweza kuwashinda wanyama wengine. Kutokana na umbile lake, alijigeuza rangi ya kijani na kujiweka nchani mwa tawi lililokaribu na njia. Alifanya hivyo ili akipita mnyama wa mwanzo aweze kujitia mkiani mwake ili afike mwanzo. Kwa bahati paa akawa mnyama wa kwanza kupita. Alijirusha na kujifunga katika mkia wa paa. Walipofika paa aliruka kutaka kukalia kiti, lakini kinyonga alilia na kudai nafasi ni yake kwani amefika mwanzo.*
>
> **Chanzo:** Bi Sharifa (Mtoni).

**ii) Ngano za mazimwi**

Hizi ni ngano ambazo wahusika wake ni mazimwi ambao wanachukua nafasi kubwa sana. Aghlabu ngano hizi hutumiwa kuonesha ulafi, tamaa, uovu na kadhalika. Ngano kama hizi zipo nyingi na hutumiwa kuonesha mambo ambayo Wamitila ameyaeleza. Kwa mfano Ngano ya Zimwi kiambatanisho 4 kutoka katika jamii ya

Wazanzibar inaonesha tamaa na ulafi wa zimwi dhidi ya mwanafunzi wake. Mwanafunzi hakulitambua hilo na kwa hiyo alimaliziwa kila chake na zimwi ambaye alijifanya mwalimu wa chuo (madrasa).

**iii) Ngano za mtanziko**

Hizi ni ngano ambazo muhusika mmoja hasa mkuu anajikuta katika hali fulani ya kushindwa kuamua atafanya nini. Kimsingi, ngano hizi zimekusudiwa kumsaidia msikilizaji au mwanajamii kukuza uwezo wake wa kufikiri na kusuluhisha mambo. Hadithi ya Mnara wa Baba na Mama muhusika mkuu ambaye ni mtoto aliyeondokewa na mama yake na kupata madhila na manyanyaso ya mama wa kambo, anafikwa na masaibu makubwa kiasi ambacho msikilizaji hujiuliza mwisho wa mtoto huyu utakuwa ni upi? Pia katika ngano ya Rajab inaonesha masaibu ya vitisho vya jini anayoyopata Rajab kiasi ambacho msikilizaji hawezi kuamini kuwa Rajab angeweza kunusurika. Hadithi inasema:

> *Ndege akaja, akaja, akaja, akaja hata akafika karibu*
> *ya nyumba. Akajigeuza kuliko nyumba.Rajab katulia*
> *juu ya kiti cha enzi anatizama miujiza tu, mara akajigeuza*
> *mtu mrefu sana asiye na mwisho, mara akajigeuza moto*
> *mkubwa unawake, hata mwisho akajigeuza umbo la*
> *binadamu akaingia ndani ya nyumba akamsogelea*
> *Rajab kisha akamtolea salamu. Huyu ni jinni.*
>
> **Chanzo:** *Fasihi Simulizi Zanzibar* (1983:84)

**4.3 Mfumo wa Ngano kabla ya maedeleo ya Teknolojia**

Kabla ya kukua kwa maendeleo ya teknolojia hasa ya maandishi na habari, utafiti huu umebaini kuwa ngano zilikuwa na mifumo yake katika utungaji, uwasilishaji, usambazaji, uhifadhi na dhima. Mifumo hiyo inafafanuliwa kama ifuatavyo:

### 4.3.1 Utungaji wa Ngano

Ngano zilitungwa papo kwa papo. Maandiko mbali mbali na wahojiwa wamebainisha kuwa watambaji wa hadithi hizi walibuni kisa kutokana na matakwa ya mahali walipo. Kwa kawaida watoto walikusanyika na kuomba kutolewa hadithi kwa bibi au babu.Wazee hao waliangalia kosa ama ni jambo gani ambalo limetokea na kutaka kulikataza au kulirekebisha. Katika utungaji kulizingatiwa rika la wanaosimuliwa ngano hiyo. Lugha ya watoto wadogo katika hadithi hiyo hiyo, ilitafautiana na lugha ilyotumika kuwasimuli watoto wakubwa. Vile vile, mtambaji aliweza kubadilisha maudhui ya hadithi yake wakati anaendelea na usimuliaji. Mtambaji anaweza kuonesha furaha au huzuni katika utoaji wa hadithi hizo. Mara nyingi ngano ambazo wahusika wake ni wanyama huwa fupi na zile ambazo wahusika wake ni binadamu au mchanganyiko huwa ndefu. Haya yanathibitishwa na Madumulla (2009: 91) aliyemnukuu Ruth Finnegan kama ifuatavyo:

> *Ngano zile ambazo zina wahusika binadamu ni ndefu zaidi kuliko ambazo zina wahusika wanyama. Kwa hakika, katika jamii nyingi zenye ngano,zile ngano ambazo hutumia wanyama kama wahusika, zimejengwa kivisasili,huku zikijaribu kuchunguza na kudadisi kwa nini namna fulani ya maisha iko kama ilivyo. Na huwa ni masimulizi mafupi tu.*

Hadithi kama hizi zipo nyingi katika jamii ya Zanzibar. Moja miongoni mwa hizo ni *Kisa cha Jongoo na Nyoka.* Ngano hii ni kisaasili ambayo haina mawanda mapana katika usimuliaji wake. Tukio ni moja tu na hata wahusika wenyewe ni wachache. Mandhari yake pia hayana upana. Ni kisa tu ambacho kina nia ya kuhoji kwa nini nyoka hana miguu na jongoo hana macho.

### 4.3.2 Uwasilishaji

Data nyingi zilizopatikana zinadhihirisha kuwa ngano ziliwasilishwa kwa njia ya ana kwa ana kati ya hadhira na fanani. Ziliwasilishwa kwa mdomo. Wakati wa uwasilishwaji wa hadithi hizo, mtambaji alifuatisha na matendo ambayo yaliwashirikisha hadhira yake. Hadhira ilisikiliza hadithi lakini inapotokea kuwa kuna mambo ya kutenda pamoja basi wote walitenda. Ushirikishwaji ni dhana pana katika kuwasilisha ngano. Ushiriki ulijumuisha mambo mbali mbali kama vile kutumia viungo kuashiria jambo. Viungo kama vile mikono ilitumika kuashiria jambo au kuelekeza. Uso ulitumika kuonesha ishara ya kufurahi, kukubaliana na jambo, mfano kwa kupandisha nyusi kuonesha waswasi juu ju ya jambo fulani; mabega yalitumika kuonesha kukataa jambo.

Miongoni mwa matendo ambayo hadhira walishirikiana na fanani ni pamoja na nyimbo, kuuliza maswali na kuyajibu; ikiwa hadhira hajafahamu aliruhusiwa kuomba sehemu aliyoikosa

kurejewa. Vile vile hadhira iliweza kushiriki kwa kuonesha hisia zake na vipi hadithi hiyo imemgusa; kwa mfano, anaweza kuonesha furaha, huzuni au kuchukizwa na jambo ambalo linasikitisha, Hali hii hujidhihirisha katika uso wa fanani na hadhira. Tukimuangalia Songoyi (1997:14) anasema kuwa katika usimuliaji wa hadithi, hadhira inaweza kushiriki katika njia tofauti. Kwa mfano anasema kuwa Waswahili wana namna maalumu ya mianzio ya ngano zao ambapo fanani humshirikisha hadhira. Hadithi huanza:

*Hadhira: Paukwa!*

*Fanani: Paukwa!*

*Aliondokea chanjagaa………..*

*Hadhira: Kajenga nyumba kakaa…….*

*Fanani: Mwanangu Mwana Siti…………..*

*Hadhira: Kijino kama chikichi……..*

*Fanani: Cha kujenga vikuta*

*Hadhira: Na vilango vya kupita*

Na hapo mtambaji huendelea kusimulia hadithi. Aidha, kutilia mkazo maneno hayo, Bi Asha (Muhadhiri wa SUZA) katika mahojiano yaliyofanyika 28/05/2015 anafafanua kuwa mtambaji huonesha matendo kulingana na mazingira ambayo hadithi inasimuliwa. Aidha hadhira anaweza kuhojiwa na fanani juu ya dhima ya ngano aliyoisikiliza na hapo hadhira hutoa maelezo namna alivyoifahamu ngano hiyo. Maneno haya yanaungwa mkono na Mulokozi (1996) ambaye anasisitiza kuwa wasikilizaji ndiyo ambao hushiriki na kuhakiki sanaa inayowasilishwa na fanani.

**4.3.3 Uhifadhi wa ngano**

Utafiti huu umebaini kuwa ngano za Zanzibar zilihifadhiwa kichwani (akilini) na pia wapo walisema kuwa zilikuwa zinahifadhiwa moyoni. Wanafunzi pamoja na wazee wamebainisha kuwa kulikuwa hakuna asasi wala hakuna njia nyengine ambayo ilitumika kuzihifadhi ngano hizo. Kwa mfano Bw. Muhammed wa Mwanyanya amesema; "*Sina kumbukumbu lakini zilihifadhiwa kichwani*." Naye Bi Aziza (ameshatajwa) amesema kuwa "*hadithi hizo zilihifadhiwa moyoni*." Kutokana na dondoo hizi utafiti huu umegundua kuwa ngano zilihifadhiwa akilini na moyoni kwa wakati huo. Hali hii iliwawezesha watambaji ngano hizo waweze kubadilisha baadhi ya mambo aidha kwa kupunguza ama kuongeza vitu kulingana na wakati na mazingira hadithi inaposimuliwa. Na hapa ndio Waswahili waliposema; *Hadithi ina ncha saba.* Kwa maana kwamba inaweza ikasimuliwa na watu tofauti huku ikibadilika baadhi ya mambo ingawa maudhui yanaweza yasibadilike.

### 4.3.4 Usambazaji

Usambazaji ni ile hali ya hadithi kutoka sehemu moja hadi nyengine. Hadithi za ngano za jamii za watu wa Visiwa vya Unguja na Pemba ziliingiliana na kufanana kutokana na kuwa watu wa jamii hizi wanahama hama wamebainisha kuwa watoto wanaposimuliwa hadithi na wazee wao, huzisambaza kwa kuwasimulia wenzao wengine wanapokutana madrasa, skuli au katika michezo yao. Bi Sharifa (ameshatajwa) anasema:katika pirika za kujitafutia maisha. Usambazwaji huo ulifanywa kwa njia ya mdomo. Wahojiwa

> *Mimi binafsi mpaka sasa huwakusanya wajukuu*
> *Zangu nikawasimulia hadithi ninapoona wanakwenda*
> *mwenendo usiotakiwa. Wanapokwenda skuli huwasimulia*
> *wenzao, au mwalimu akisema mwenye hadithi awatolee wenzake*
> *basi husimama na kutoa hadithi wenzao wakasikiliza.*

Kutokana na maelezo hayo, imeonekana kuwa ngano zilirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya mdomo.

### 4.3.5 Dhima ya ngano

Wazee walisimulia watoto wao hadithi wakiwa na dhamira zao. Kazi hizi hazikutolewa bure ila kulikuwa na mambo ambayo vijana walitakiwa wayapate. Mambo hayo ndiyo yaliyoweka misingi ya mila, silka na desturi ambazo zilikubalika katika jamii. Kwa hivyo dhima za ngano hizo ni pamoja na:

#### 4.3.5.1 Kuelimisha

Katika dhima hii, hadithi ilikuwa ni chuo ambacho watoto walijichotea taaluma inayohusiana na nyanja mbali mbali za maisha. Kwa mfano, walijifunza namna ya kuishi watu vizuri, kupendana, kusaidiana, kuhurumiana na hata elimu inayohusiana na umuhimu wa kumuabudu Mola wao. Vile vile baadhi ya wahojiwa wanaona

kuwa hadithi zilitumika kufundishia mila na tamaduni za Kizanzibari. Tamaduni hizo ni kama vile heshima, namna ya mavazi, adabu za kula, ibada, matambiko, maombi na kadhalika.

Hadithi inayoitwa *Mcheka Kilema* inawafunza watoto namna ya kuheshimu watu wengine na pia kuwa na uvumilivu katika kutoa maamuzi. Katika hadithi hii, watoto waliweza kujifunza kuwa walipaswa kuwaheshimu watu waliomo katika jamii hata kama wana kasoro za maumbile (walemavu), kwani kukosa heshima kunaweza kuwa ni sababu ya mtu kukosa alilolikusudia kama walivyomkosa mke wale vijana ambao walimcheka yule bibi kwa ulemavu aliokuwa nao. Pia katika hadithi hii watoto wanapata kujifunza subira pamoja na kuheshimu mila na desturi za jamii. Kwani kwa utamaduni wa Zanzibar kijana anapotokea mchumba ni lazima achunguzwe tabia na wazee, iwapo wazee wataridhia ndiyo kijana ataolewa. Kupitia kijana wa kike katika ngano hii ndiyo unapatikana ujumbe huo.

#### 4.3.5.2 Kuburudisha

Ngano zina dhima ya kuburudisha. Utafiti huu umegundua kuwa watoto walikuwa wanakusanywa kutolewa hadithi kwa lengo la kuwafurahisha na kuwaondoshea machofu ya mchana kutwa. Burudani hasa inakuja wakati wanaposhirikishwa katika hadithi hizo. Kwahivyo kuimba, kushangiria, kuhoji na kupewa majibu yaliwafanya watoto wajisikie faraja na hivyo kufurahi katika nafsi zao. Baadhi ya wahojiwa wanasema kuwa kutokana na uzuri wa hadithi hizo, walikuwa wakiomba watolewe hadithi nyengine kwani ziliwafurahisha.

#### 4.3.5.3 Kuasa

Ngano zilitolewa kama ni njia mojawapo ya kuwaasa, kuwatahadharisha, kuwakanya na kuwakosoa watu wenye tabia mbaya katika jamii. Tabia za choyo,

fitna, chuki, ubinafsi, umbea, wivu, wizi na nyenginezo zinaonekana kuleta maafa kupitia ngano za Zanzibar. Kwa mfano kuna ngano nyingi zinazohusiana na chuki na ubinafsi unaofanywa na mama wa kambo dhidi ya mtoto wa mume wake na madhara ya chuki hizo. Pia kupitia ngano za Fisi na Sungura tunaona ubaya wa ulafi wa fisi na kadhalika. Hadithi hizi zinatoa vitisho kwa watoto kwa kuonesha maafa au hasara inayopatikana kwa kuwa na tabia kama hizo. Maelezo ya Bi Sharifa anayosema kuwa watoto walitolewa hadithi baada ya kuonekana na tabia isiyoridhisha, yaathibitisha ukweli huo.

#### 4.3.5.4 Kurithisha Amali za Jamii

Katika utafiti huu wanafunzi waliofanya majadiliano, wameeleza kuwa ngano zinarithisha amali za jamii. Katika jamii ya watu wa Zanzibar kuna amali mbali mbali ambazo hujitokeza katika ngano. Miongoni mwa amali hizo ni uvuvi, kilimo, uwindaji, useremala, na biashara. Kwa mfano katika hadithi *Mcheka Kilema*, inaonesha kuwa moja kati ya amali zinazofanywa Zanzibar ni kilimo. Katika hadithi ya *Mtendazema*, watoto wanapata kuelewa kuwa amali za jamii za Zanzibar ni pamoja na ushoni kwani katika kijiji hicho alikuwepo fundi cherahani. Kwa hiyo ngano hizi zinaonesha kuwa kilimo na ushoni ni miongoni mwa amali za jamii.

## 4.4 Teknolojia Inayotumika Kuwasilisha, Kuhifadhi, na Kusambaza Ngano Zanzibar

Ulimwengu ni kitu ambacho kinabadilika. Kadiri siku zinavyokwenda binadamu hujitafutia njia rahisi za kuweza kupambana na maisha yake na hivyo kupata muda wa mapumziko. Kwa mujibu wa Songoyi (997:22-25) anaeleza kuwa mwanadamu amepitia mifumo mitano ya maisha. Kila mfumo ulikuwa na mabadiliko yake ambayo yalikuwa ni bora zaidi ukilinganisha na mfumo uliopita nyuma.

Zanzibar ni moja kati ya jamii ambayo iliingiliwa na wageni mbali mbali. Kwa sasa Zanzibar imepiga hatua katika utumiaji wa teknolojia ya uandishi na habari. Wasanii katika jamii hutumia teknolojia ya habari na uandishi katika kuziwasilisha, kuhifadhi na kusambaza hadithi za ngano. Miongoni mwa teknolojia ambazo hutumika Zanzibar ni kama zifuatavyo:

### 4.4.1 Redio

Wahojiwa wengi wamesema kuwa kupitia redio huweza kusikiliza hadithi kupitia vipindi vya watoto. Redio ni kifaa ambacho hutumia CD au kanda za kunasia sauti. Baadaye sauti hizo kurushwa hewani kupitia mawimbi ya sauti. Redio huhitaji kupatikana kwa nyenzo ya umeme au betri ndipo iweze kusikika. Katika visiwa vya Zanzibar, kuna vituo vingi vya redio. Kuna vile inavyomilikiwa na serikali kupitia *Shirika la Utangazaji Zanzibar* (ZBC). Hapo mwanzo ilijulikana kwa jina la *Sauti ya Tanzania Zanzibar.* Kituo hiki kinafanya kazi ya kupita maskuli kurikodi vipindi vya watoto, katika vipindi hivyo kunatolewa vitendawili, mafumbo na ngano. Kipindi hiki kiliitwa *Chechei shangazi/ mjomba.* Kipindi hiki kinarushwa hewani kila siku ya Jumapili alasiri. Pia kupitia ZBC kuna kipindi cha *Tucheze Tujifunze*; Hiki ni kipindi kinachoandaliwa kupitia mradi wa "Rise". Lengo la mradi ni kuzitumia ngano kwa kufundisha sarufi ya Kiswahili kwa watoto. Kutokana na uhuru wa habari, sasa kuna vituo vingi vya redio kama vile Zenj Fm kukiwa na kipindi cha "Totos Conner".

### 4.4.2 Maandishi

Maandishi ni aina ya teknolijia ambayo katika visiwa vya Zanzibar imeanza baada ya majilio ya wageni hasa Waarabu. Kwa mujibu wa Ingrams (1967: 77) anasema kuwa wageni wa mwanzo walioingia Zanzibar walianzisha misikiti ambamo wenyeji

walijifunza kusoma na kuandika. Kwa mfano anasema kuwa msikiti wa Kizimkaziuliojengwa 1107 AD na ule wa Msuka (Pemba) uliojengwa 1414 ilitumika kuwafundisha watu. Waarabu waliwafundisha watu namna ya kuandika katika vyuo vya Kuran. Kama ilivyoelezwa kuwa waarabu walikuja na hadithi za *Alfu Lele U Lela* ambazo zilikuwa katika mfumo wa maandishi; hali hii ilikuja kuathiri ngano za Zanzibar. Ingrams (1997: 350) anafafanua kuwa hadithi nyingi zilizomo katika jamii ya Zanzibar zinafanana na zile za *Alfu Lela U Lela* na ni vigumu kuzibagu ipi inatoka katika jamii ya Zanzibar. Ingrams ni mgeni ambaye ameandika ngano nyingi kwa lugha ya Kiingereza katika kitabu chake *Zanzibar Its History and Its People* (1967). Baadae walipokuja watawala wa Kiingereza wakaanzisha elimu ya darasani na kushajiisha uandishi wa kazi za fasihi ngano ikiwa ni moja kati ya kazi hizo kama anavyodai Rajmund (1991: 1) kuwa ilipoonekana kuna upungufu mkubwa wa kazi za fasihi katika maandishi shirika la East African Publishing House ndipo lilipoanza kuchapisha ngano 1975. Kwa mujibu wa Mw Ali Mwalimu (SUZA) anaeleza kuwa ngano za Zanzibar zilikusanywa na mtafiti Bi Brigiki na kuziandika kupitia kitabu chake kiitwacho *Paukwa za Zanzibar.* Mpaka ripoti hii inawasilishwa kitabu hiki kimekosekana. Aidha kupitia SUZA ambayo hapo awali ilijulikana kama TAKILUKI wanajishughulisha kukusanya na kuziandika ngano za Zanzibar. Kitabu ambacho kimechapishwa hadi sasa kinaitwa *Fasihi Simulizi ya Zanzibar* (1983) na kuchapishwa tena mwaka (2007). Kitabu hiki kimekusanya ngano kama vile *Kijoka Sindano* (uk 43- 44), *Simba na Makame wa Makame* (uk 41- 42), *Mtendazema* (uk 80- 82).

Pia Mw Ali anasema, ametoa kitabu cha *Utenzi wa Kunguru na Bata.* Ngano hii inayohusiana na kisa cha kunguru na bata; Kunguru katika kisa hiki anaigiza mwenendo wa bata katika kula, lakini kutokana na vishindo na papara zake

anashindwa na kwa hiyo kuendelea kuwa mkondefu maisha. Ulafi na kutokujali ndiyo chanzo cha ukondefu wake. Kitabu hiki kimeandikwa kwa njia ya utenzi. Pamoja na hayo baadhi ya wazazi wamedai kuwa hata watoto sasa hivi wanaposimuliana hadithi huchukua kalamu na karatasi au hata kuchora picha zilizomo katika hadithi inayosimuliwa; kwa mfano huchora picha ya muhusika, nyumba, njia, msitu na kadhalika.

### 4.4.3 Kanda za video na CD

Kanda za video hurekodi picha ya mtu na matendo yake pamoja na sauti. Picha hizo ili ziweze kuonekana huoneshwa kwenye kioo cha televisheni. Kupitia televisheni watu huweza kujifunza ngano kwa kuigizwa na watambaji kama mchezo wa kuigiza au kupitia kipindi cha "watoto show" cha ZBC TV.  Watangazaji huwakusanya watoto kutoka maeneo mbali mbali na kutoleana hadithi.

### 4.4.4 Kompyuta

Kwa mujibu wamtandao wa WWW. Shuledirect. Co.tz, wanadai kuwa hii ni teknolojia ambayo imeanza miaka ya karibuni baada ya watu kujua kutumia kompyuta. Kupitia kifaa hiki wasanii huziingiza ngano katika programu na kuzihifadhi kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Programu hizo hutumika pale zinapohitajika tu; kwa mfano katika kufundishia au kufanya utafiti unaohusiana na ngano.

## 4.5 Athari za Teknolojia katika Kutunga, Kuwasilisha, Kuhifadhi na Kusambaza Ngano

Kukua na kuendelea kutumika teknolojia katika kutunga, kuwasilisha, kuhifadhi na kusambaza ngano Zanzibar kumeweza kuleta athari chanya na hasi. Watoaji taarifa wamezielezea athari hizo kama ifuatavyo:

### 4.5.1 Athari Chanya za teknolojia katika kuwasilisha, kuhifadhi, kusambaza na dhima za Ngano

Katika kulijadili suala hili maandiko na wahojiwa wengi wametoa mawazo yafuatayo;

**Kudumu kwa muda mrefu**

Kazi za sanaa zinapohifadhiwa kupitia teknolojia zilizoainishwa hapo juu, huweza kudumu kwa muda mrefu zaidi ukilinganisha na kuhifadhiwa kichwani kama ilivyozoeleka. Kwa mujibu wa wahojiwa ambao walitoa mawazo yao, wameeleza kuwa njia ya maandishi hudumu zaidi kuliko CD na tepurikoda. Kudumu kwa kazi hizi kunasaidia kusambaa katika eneo kubwa na kuwafikia walio wengi. Vile vile huweza kueka kumbukumbu na hivyo vizazi vinavyokuja kuelewa utamaduni wa jamii ya Wazanzibari. Maandishi husaidia kuhifadhi utamaduni wa jamii kwa vizazi na vizazi kama anavyofafanua Songoyi (1997: 31-32). Vile vile mmoja kati ya wazee alitoa maelezo kuwa wanatumia njia za kuhifadhia ngano ili zisipotee kabisa kabisa. Kwa sasa ngano nyigi zinapatikana katika vyombo hivi kuliko katika vichwa vya watu. Kwa upande wa watoto ngano hizo huzipata kupitia katika vitabu wanavyosoma skuli kwa vile ni moja kati ya somo katika mtaala wa elimu.

Vile vile TAKILUKI kwa sasa SUZA ni miongoni mwa asasi ambazo zimekusanya hadithi za ngano na kuziandika. Bi Asha mwalimu wa SUZA amesema kuwa, watafiti wao walipita kila wilaya na kurikodi kwa kanda za kunasia sauti na baadaye kuziandika. Haya maandishi yamedumu hata leo hii. Moja kati ya ngano hizo ni ngano ya Sudi iliyo katika kiambatanisho namba 2.

**Kuzidi Ushiriki**

Teknolojia ya habari imewawezesha watoto kupata kushiriki katika uwasilishai wa usimuliaji wa ngano. Wahojiwa walisema kuwa sasa watoto ambao wanaangalia televisheni wanapata fursa ya kushiriki kwa kupiga simu. Vile vile watoto kutoka sehemu mbalimbali hukusanywa ZBC TV na kusimulia hadithi katika kipindi cha "watoto show." Kwa mujibu wa wafanyakazi wa shirika hilo wamesema kuwa wakati wa kurikodi kipindi hicho huwa wanatoa fursa kwa watoto ambao wapo nyumbani kushiriki kwa kutoa maoni yao au kusimulia hadithi zao. Ushiriki huo unaweza kuwa wa kuuliza maswali, kupongeza, au kuongezea pale kwenye kasoro.

Pia kwa zile ngano ambazo zimetambwa, fundi mitambo hutengeneza sauti au mlio ambao huleta mguso zaidi kwa mtazamaji wa televisheni kuliko ikisimuliwa kwa mdomo. Kwa hali hii zinazifanya ngano hizo kupata uhai katika uwasilishwaji wake. Pamoja na hayo hata watu wazima hupata nafasi ya kushirki kwani huangalia vipindi hivyo, na hata watu wa jamii nyengine nje ya Zanzibar wanapata kushiriki na kwa maana hiyo na hata usambazaji huongezeka kupitia vipindi hivyo. Pia watoto wanaposimulia kwa kuchora picha zinazoonesha matokeo katika hadithi, huongeza ushiriki wa watoto; kwa mfano wanaweza wakasifu, kukejeli picha au hata kukosoa na kufanya marekebisho.

**Kuzaa tanzu za fasihi andishi**

Kuja kwa maandishi na ngano kuanza kuandikwa, baadhi ya wasanii walipiga hatua zaidi na kuziandika kwa usanii zaidi na hapo zikazaa hadithi fupi. Watoa taarifa wa SUZA Bi Asha na Mw. Ali wanaunga mkono hoja hii. Kwa mfano TAKILUKI (1981) wametoa kitabu chenye mkusanyiko wa hadithi fupi 37. Hadithi hizi zilibuniwa kutoka katika ngano, mifano ya hadithi zilizomo ni kama vile *Asali*

*Chungu*, *Ulimi wa Damsimu* na *Thamani ya Punda.* Hadithi hizi fupi ndiyo ambazo zimezaa riwaya za Kiswahili; Kwa mfano hadithi fupi ya *Asali Chungu* imetoa jina la riwaya ya *Asali Chungu*. Pia kwa mujibu wa Mw. Ali Mwalimu (SUZA) anasema kuwa teknolojia ya uandishi imewezesha kuwasilisha na kuzihifadhi ngano katika mfumo wa utenzi; Yeye ametunga utenzi kutoka katika ngano inayoelezea kisa cha *kunguru na bata.* Katika kisa hiki, kunguru anataka kumwiga bata namna anavyokula; hata hivyo anashindwa kwani yeye hakuzoea kula taratibu kama anavyokula bata. Kutokana na tabia yake hiyo kunguru hanenepi hadi leo.

**Zimekuwa ni nyenzo ya kufundishia madarasani**

Kutokana na kuwa ngano ni nyenzo ya kuwapatia watoto taaluma tokea hapo zamani, sasa inaonekana kutumika katika taasisi rasmi kama vile skuli na vyuo. Hapo awali zilitumika kwa njia ambazo si rasmi. Mtaala wa elimu imeziingiza ngano katika somo la Kiswahili si tu kwa kufundisha fasihi simulizi ya Kiswahili, bali pia kufundishia isimu ya lugha hiyo. Kwa mfano watoto hujifunza aina za maneno, ufahamu na kadhalika.

Mmoja kati ya waandishi (jina limehifadhiwa) alipohojiwa alisema kuwa Zanzibar imeanzisha mradi unaoitwa “Rise.” Mradi huu ni mahsusi kwa kutoa mafunzo kwa watoto wadogo kupitia ZBC redio. Waalimu hurikodi hadithi na baadaye kuzirusha katika redio. Watoto hao ni wa nasari hadi darasa la pili. Kipindi kinajulikana kwa jina la *Tucheze tujifunze*. Katika kufundisha lugha hutumia ngano na baadae kutoka katika ngano hiyo watoto hufundishwa jambo lilokusudiwa.

**Huhifadhi utamaduni wa jamii kwa ajili ya vizazi vijavyo**

Baadhi ya wahojiwa na maandiko yaliyopitiwa yanasema kuwa kitu kinapoandikwa huwa na athari ya muda mrefu kuliko kinachosimuliwa. Hivyo kuziandika

kumewezesha kuzihifadhi mila, silka na desturi za Wazanzibari ambazo zinaonekana kupotea kwa kasi katika ulimwengu huu wa utandawazi. Pia kuhifadhiwa huku kunazifanya ngano ziweze kuwafikia walio wengi. Kwa mfano ngano ambazo zimo katika vitabu vya kufundishia watoto skuli, vinawafikia watoto walio wengi hata ambao si watu wa jamii hiyo. Pia kitabu cha *Fasihi Simulizi Zanzibar* (1983) na kitabu cha *Zanzibar Its History and Its People* (1967) ambavyo vinasomwa na wanafunzi wanaosoma fasihi, vimeweza kusomwa na watu wengi wakiwemo wa vyuo vikuu na kwa hiyo kupata eneo kubwa la wasomaji. Watu hawa wote huweza kufahamu tamaduni za Wazanzibar kupitia ngano hizo.

### 4.5.2 Athari hasi za Teknolojia katika Kuwasilisha, Kuhifadhi na Kusambaza Ngano

Utumiaji wa teknolojia katika jamii una manufaa makubwa kama tulivyoona kabla, lakini pia kuna matatizo yanayotokana na utumiaji wa teknolojia. Katika muktadha wa ngano, licha ya manufaa hayo kuna baadhi ya matatizo ambayo huzikabili ngano zinapowasilishwa, kuhifadhiwa ama kusambazwa kwa kutumia teknolojia zilizoainishwa katika utafiti huu. Miongoni mwa athari hasi ambazo utafiti huu umezibaini ni hizi zifuatazo:

**Msomaji husoma kwa hamasa zake tu**

Utafiti huu umebaini kuwa ngano zinapowasilishwa, kuhifadhiwa ama kusambazwa kwa njia ya maandishi (vitabuni) au kompyuta, msomaji husoma kwa hamasa/ hamu yake tu. Wahojiwa walio wengi wamesema kuwa uwasilishwaji huu wa ngano haumfanyi mtu kusoma kwa sababu kaguswa au kuvutiwa na jambo fulani katika ngano hizo. Baadhi yao wamesema kuwa ngano zilizoandikwa husomwa zaidi na wasomi kwa ajili ya kuhakiki kazi hizo. Wamesema hivyo kwa sababu msomaji

haoneshi kuguswa na matokeo yaliyomo katika hadithi hizo. Ama kwa upande wa wanafunzi wa skuli za msingi na sekondari wao huzisoma kwa sababu ni moja kati mada zao wanazotakiwa kuzisoma.

**Kukosa uhalisia**

Hii ni athari ambayo imegusiwa takriban na kila aliyetoa taarifa katika utafiti huu. Maandiko mbalimbali nayo yamegusia jambo hili. Kukosa uhalisia ni dhana pana ambayo imeanza tokea utungaji, uwasilishaji, uhifadhi, usambazaji na hata dhima.

Katika utungaji kuna mambo ambayo kama vifaa vya kiteknolojia vikitumika huwa havionekani. Kama ilivyoelezwa hapo kabla kuwa ngano zilibuniwa na kutungwa kulingana na muktadha, katika mkabala huu, ngano inakuwa haiwezi tena kubadilika kulingana na mahitaji na wakati uliopo. Hapa inamaanisha kuwa ngano huwa imepata umbo la kudumu. Hii ni kinyume na ile kanuni ya kuwa *hadithi ina ncha saba*. Umbo ambalo haliwezi kubadilika kwa vizazi na vizazi mpaka msanii atakapoamua kuandika tena upya.

Pia fanani na hadhira wanakosa kuonana uso kwa uso; mathalan kupitia redio, fanani husikia sauti tu, aidha katika maandishi na kompyuta fanani haonekani; kitu ambacho ni kinyume kabisa na sifa ya ngano. Uwasilishaji wa ngano kwa kutumia teknolojia za habari na uandishi husababisha baadhi ya mambo kufa mojo kwa moja. Katika uwasilishaji hadhira hawezi kushiriki katika matendo kama vile kuuliza maswali, kuimba, kupiga makofi, kuonesha furaha au hamu ya kutaka kujua kitakachoendelea kwa muhusika na kadhalika.

Vile vile kwa kutumia maandishi ama kompyuta kuwasilisha ngano kuna baadhi ya mambo yanakosa kuandikwa. Kwa mfano baadhi ya ishara, miguno, matendo ya fanani; huwa haviandikiki. Katika ngano mwandishi hakuonesha namna sauti ya

simba ilivyokuwa; mihemo na mingurumo yake. Mfano tunaweza kuambiwa tu simba ametoa sauti kali. Kwa kuambiwa hivyo mtu hawezi kupata hisia ya kuogopa au kupata athari yeyote ile. Katika ngano ya *Mnara wa Baba na Mama*, iliyoandikwa katika kiambatanisho namba 1, baadhi ya ishara hazionekani; kwa mfano namna ndege anavyodonoa mtama au namna ng'ombe anavyofunua mdomo. Kukosekana kwa ishara hizi kunazifanya ngano kupungua au kukosa kabisa uhalisia wake. Pamoja na yote hayo kuna waliosema kuwa kutokana na kuja kwa vifaa hivi, na watoto kujishughulisha na masomo ya skuli na tuisheni watoto hawana muda wa kusikiliza ngano. Hali hii inazifanya ngano hizo kutoweka katika jamii na dhana yenyewe pia kupotea kabisa.

**Kupotea au Kuharibika kwa vifaa vyenyewe**

Utafiti huu umebaini kuwa ngano zinapohifadhiwa katika mfumo wa kiteknolojia ni rahisi kupotea. CD, tepurikoda na kanda za video ni vitu ambavyo havichukui muda mrefu kuharibika. Kwa hali hiyo, iwapo ngano zitahifadhiwa katika vifaa hivyo bila ya uangalifu na kuwa makini, zinaweza kupotea kabisa. Walimu kutoka SUZA (Bi Asha na Mw. Ali) walisema kuwa wakati wa kukusanya hadithi, walipita kila wilaya na kurikodi. Baada ya hapo zikaandikwa. Kwa sasa zile kanda hazionekani na hizo zilizopatikana zimeshaharibika. Kwa upande wa watangazaji nao wamedai kuwa kanda za video baada ya kukaa kwa muda huganda wakati wa kuzirusha. Hali hii huzifanya ngano zilizohifadhiwa kwa kurikodiwa katika kanda za video, CD, na vinasa sauti kukosa maisha marefu.

**Wanaofaidika ni wachache**

Utafiti huu umebaini kuwa mara nyingi ngano ambazo zimewasilishwa na kuhifadiwa katika teknolojia zilizoainishwa, huwanufaisha watu wachache. Redio ni

kifaa hiki kinahitaji betri au umeme ndipo kiweze kufanya kazi. Jamii ya watu walio wengi huikosa fursa hiyo kwa vile hawana uwezo wa kumiliki kifaa hicho. Pia muda wa kurushwa vipindi hivi mara nyingi ni muda ambao watu wana shughuli zao, hivyo wanakuwa hawana muda wa kusikiliza. Kwa upande wa vitabu, kompyuta na kanda za video ni ghali na vinahitaji utaalamu. Mathalani kuandika na kompyuta ni teknolojia ambazo zinahitaji mtu kujua kusoma na kundika na pia utaalamu wa kujua kuitumia kompyuta. Kwa mujibu wa wahojiwa wamekiri kuwa Wazanzibari walio wengi hawana ujuzi wa kutumia kompyuta, isipokuwa wale ambao wamepata fursa ya kusomea kompyuta. Pamoja na hayo, watu wengi hasa walio tabaka la chini hawana utamaduni wa kusoma vitabu. Kwa hivyo, watu hawa hawawezi kuzijua ngano hizo na kwa hiyo kubaki kuwa ni mali ya wasomi na wenye utamaduni wa kusoma maandiko hayo.

Pamoja na hayo, utafiti huu umebaini kuwa watu walio wengi hujihusisha zaidi na kuangalia filamu au watoto kucheza mchezo kwenye kompyuta kuliko kusikiliza ama kuangalia ngano; hasa sehemu za mjini. Kutokana na mambo hayo hata zile dhima za ngano huwa haziwafikii walengwa ambao ni jamii ya Wazanzibari. Katika jamii ya Wazanzibar kwa sasa imeacha maadili yao na imeathirika na tamaduni za nje hasa zile za magharibi. Uhalisia huu umekuja kutokana na dunia kwa wakati huu kuwa katika mfumo wa utandawazi; hivyo Wazanzibar, kwa sababu wao ni sehemu ya dunia, nao wameacha tamaduni zao ambazo zimo ndani ya fasihi yao huku ngano ikiwa na nafasi kubwa ya kuzihifadhi mila na desturi hizo. Zikiangaliwa athari hizi hasi, utafiti huu unaungwa mkono na maneno ya Khamis (1983: 3) ambaye anasema:

*Fasihi simulizi imevizwa kwa maendeleo ya*
*kiufundi na uvumuzi wa mashine kadhaa has*
*za uchapaji na za mawasiliano hasa redio,*
*tepurikoda na televisheni.*

**Kukosekana utamaduni wa kuendelea kusimuliwa ngano**

Wakati wa ukusanyaji data watu ambao walihojiwa wamesema kuwa kuzuka kwa teknolojia za habari na kompyuta kumewakosesha fursa ya kuzisikia ngano. Wengi wao wamesema kuwa hawajawahi kukusanywa kusimuliwa hadithi na hao watoto wa sasa huzipata kupitia kwa wenzao maskulini ambao kwao ni ng'ambo na teknolojia hizi bado hazijaenea kwa kiasi kikubwa. Kutokana na maelezo hayo, utafiti huu umebaini kuwa kwa siku zijazo dhana ya ngano itabakia vitabuni, kwenye CD na kompyuta. Jamii yenyewe itapoteza kabisa lengo la ngano na kwa hiyo ni kitu kigeni kusikika kwenye masikio ya watu.

**Kuwapo kwa hati miliki**

Kazi za ngano ambazo wasanii wamezihifadhi kupitia teknolijia mbalimbali zimekuwa ni milki yao. Kwa kuwa fasihi simulizi ni mali ya jamii yote, kupewa mtu ama taasisi yeyote umiliki ni kuipotezea kazi hiyo sifa yake; Kwani kazi hizi hazina mmiliki. Wahojiwa wamesema kuwa vitabu au CD na kanda za video ambazo zinatumika kuwasilishia ngano zimepewa hati miliki; hivyo haruhusiwi mtu mwengine yeyote kuichukua kazi hiyo bila ya idhini ya mmiliki. Kwa mfano *Fasihi Simulizi Zanzibar* (1983: ii) kimeandikwa kuwa kazi za fasihi simulizi zilizomo kwenye kitabu hicho, ngano ikiwa ni miongoni mwao ni milki ya taasisi ambayo imemiliki kitabu hicho, hivyo haruhusiwi mtu kuiga, kutafsiri, kutoa chapa au kukitoa kwa jinsi yeyote bila ya idhini ya shirika lililochapisha kitabu hicho. Hali hii

inazifanya ngano hizo kuwa si mali tena ya jamii kama ilivyo bali ni za asasi zinazokusanya ngano hizo.

**HITIMISHO**

Katika sura hii, matokeo ya utafit yamewasilishwa na kuchambuliwa kulingana na maswali ya utafiti. Maswali hayo yameakisi malengo ya utafiti. Mjadala umegawika katika sehemu tatu; ya kwanza imefanya mjadala unaohusu historia ya fasihi kwa jamii ya Zanzibar pamoja na chimbuko na asili ya ngano Zanzibar. Sehemu ya pili imejadili teknolojia inayotumika Zanzibar katika utungaji, uwasilishaji na kuhifadhi ngano. Sehemu ya tatu imefanya tathmini juu ya athari chanya na hasi za utumiaji wa vifaa vya kiteknolojia katika utungaji, uwasilishaji, uhifadhi na dhima za ngano. Kwa ufupi asili ya ngano ni kuwa ni nyenzo ya kuwatishia watoto ili kuacha tabia mbaya,baadhi ya watu kutaka kuonesha uelewa wa mazingira na hivyo kuyaeleza katika ngano na pia ni watu kuwa na uwezo mkubwa wa kutumia lugha na kwa hiyo kutaka kuonesha uwezo wao kwa watu wengine. Aidha chimbuko la ngano ni baada ya jamii za kale kuvumbua vifaa bora vya kutendea kazi na hivyo kupata muda mwingiwa kupumzika ambao uliwezesha kubuni ngano ambazo ziliwafariji zaidi. Ngano zilibuniwa kulingana na muktadha ambao fanani na hadhira walikuwapo, ziliwasilisha kwa kusimuliwa mbele ya hadhira. Hadhira ilishirikishwa katika matendo mbalimbali. Zilihifadhiwa vichwani na kusambazwa kwa njia ya mdomo. Dhima ya ngano ni pamoja na kuasa, kuelimisha kurithisha amali za jamii, kuburudisha na kuhifadhi utamaduni wa jamii.

Teknolojia ambazo zinatumika kuwasilisha, kusambaza na kuhifadhia ngano ni teknolojia ya uandishi, kompiyuta, CD, redio na kanda za video. Vifaa hivi vya kiteknolojia kwa upande mmoja vinasaidilia kuzihifadhi na kuziendeleza ngano

lakini kwa upande mwengine zinaonesha kudumaza ngano kama hazikutumiwa na kutuzwa ipaswavyo.

Kwa upande wa athari za kutumia teknolojia hizo, zipo chanya na hasi. Athari chanya ambazo hupatikana kwa kutumia teknolojia katika kutunga, kuwasilisha na kuhifadhi ngano ni kama vile kudumu kwa muda mrefu hasa zinapoandikwa au kuhifadhiwa katika kompiyuta, kuzidi ushiriki kupitia kanda za video, kuzaa tanzu za fasihi andishi kama vile hadithi fupi na tendi, zimekuwa ni nyenzo za kufundishia lugha madarasani na pia ni nyenzo ambayo inatumika kuhifadhi utamaduni wa jamii kwa vizazi vijavyo. Athari hasi zinazopatikana kwa kutumia teknolojia za kisasa ni msomaji kusoma kwa hamasa zake bila kuzingatia kinachoelezwa, kukosa uhalisia kwa vile hukosa sifa za ngano, kupotea au kuharibika kwa vifaa ambako hupelekea kupotea kwa hadithi zenyewe, kukosekana utamaduni wa kusimuliwa ngano katika jamii na kuwapo kwa hati miliki ambazo huizuia jamii kukosa uhuru wa kumiliki ngano hizo.

Licha ya kuwa na athari hasi ambazo zimejidhihirisha kutokana na utumiaji wa teknolojia katika utungaji, uwasilishaji, uhifahi na dhima za ngano, jamii inahitji teknolojia hizi kwa vile dunia imo katika mabadiliko na hivyo haiwezekani kubaki katika ukale. Jamii ni muhimu kuchagua teknolojia inayokwenda na wakati ambayo itaziwezesha ngano hizo kudumu kwa muda mrefu na kuwafikia watu wengi. Mambo haya yakifanyika tunategemea kuwa yatawezesha utamaduni wa kusimuliana ngano kurudi kwa wana jamii.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO LA UTAFITI

Katika sura hii, mtafiti ametoa hitimisho la kazi kwa kueleza mchakato mzima uliopitiwa katika utafiti huu. Sehemu hii imeweza kuelezea kipengele cha muhtasari wa tasnifu, Kwa kuonesha kuwa Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza Athari za Teknolojia katika Ngano Zanzibar. Tulilenga mambo matatu ambayo ni kuchunguza namna teknolojia ya habari na uandishi zinavyoathiri ngano katika utungaji, uwasilishaji, usambazaji, uhifadhi na dhima. Kwanza, kuonesha historia ya ngano katika jamii ya Zanzibar na namna zinavyoathiriwa na teknolojia. Pili, ni namna nadharia iliyotumika na ilivyomsaidia mtafiti katika kuchambua data na kuzijadili. Tatu, ni maoni na mapendekezo ya mtafiti kuhusu tafiti zijazo.

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Matokeo ya tafiti huu, umegawika katika sura tano, kila sura imejitokeza kufafanua vipengele maalum vya utafiti. Sura hizo kwa ufupi zilijitokeza kama ifuatavyo: Sura ya Kwanza inahusu usuli wa tatizo la utafiti kwa kufafanua dhana ya ngano na namna zilivyokuwa. Aidha katika surs hii, mtafiti ameeleza malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti pamoja na nadharia inayoongoza utafiti huu.

Sura ya pili, mtafiti anafafanua mapitio ya maandiko yanayohusu ngano pamoja na dhana ya teknolojia na nafasi yake katika fasihi. Maudhui hayo kwa kiasi kikubwa yamejaribu kueleza mada iliyotafitiwa. Hatimaye, maandiko yakabainisha mapengo ya kimaarifa kuhusiana na mada yetu.

Katika sura ya tatu, imeeleza kuhusu mbinu na vifaa vilivyotumika katika mchakato mzima wa utfiti huu. Vipengele vilivyojumuishwa katika sura hii ni pamoja na mpango wa utafiti, eneo lililotumika katika utafiti, jumuia ya watafitiwa na uteuzi

wa sampuli, lilielezwa kwa uwazi. Pia sura hii ilifafanua namna data zilizokusanywa zitakavyochanganuliwa katika sura ya nne. Mwisho vimebainishwa vikwazo mbalimbali mtafiti alivyokutana navyo wakati wa mchakato wa ukusanyaji na uchambuzi wa data.

Sura ya nne, imejadili matokeo ya utafiti kwa uwazi. Data zilizochambuliwa zinahusina na athari za teknolojia katika ngano; Zanzibar. Sehemu hii imegawanywa katika sehemu kuu tatu kulingana na maswali yaliyoongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza imejadili historia ya fasihi simulizi, asili na chimbuko la ngano Zanzibar pamoja na historia yake katika uwasilishaji, usambazaji, uhifadhi na dhima. Sehemu ya pili imejadili vifaa vya kiteknolojia vinavyotumika kuwasilishia, kuhifadhia na kusambazia ngano. Na sehemu ya tatu imejadili namna vifaa hivyo vinavyoathiri ngano kwa kuhusisha athari chanya na hasi.

Sura ya tano na ya mwisho, ni hitimisho la kazi kwa kueleza kwa muhtasari mchakato mzima wa utafiti hadi kufikia ugunduzi wa yote yaliyotokea. Aidha mtafiti amependekeza kuhusu mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa kuhusu tafiti zijazo.

## 5.2 Utoshelevu wa Nadharia

Katika utafiti huu nadharia iliyotumika katika kuchambua data za kazi hii ni uhalisi. Kwa vile utafiti huu ulihusu Athari za Teknolojia katika Ngano, hivyo nadharia hii ilisadifu hali halisi ya namna fasihi inavyobadilika katika jamii kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia yaliyojitokeza.

Jamii ya Wazanzibari kwa sasa imepiga hatua kubwa juu ya utumiaji wa teknolojia mbalimbali, zikiwamo za habari na uandishi. Teknolojia ya utumiaji wa kompyuta, CD, vinasa sauti, televisheni, redio na uandishi wa vitabu vimekua kwa haraka

zaidi.Teknolojia ya uandishi ni ya mwanzo kutumika kuwasilishia, kusambaza na kuhifadhi ngano. Mabadiliko ambayo yametokea katika jamii za Wazanzibari tokea kuja kwa teknolojia ya uandishi wakati wa ujio wa wageni wa kiarabu na wakoloni wengine, na baadaye kufuatiwa na teknolojia ya habari yameweza kuleta athari chanya na hasi katika ngano na fasihi simulizi.

Nadharia imeweza kumsaidia mtafiti kutathmini hali ya ngano ilivyokuwa kabla ya maendeleo ya teknolojia ya uandishi na habari na namna ilivyobadilika baada ya kuja na kukua kwa maendeleo hayo. Maendeleo haya ya teknolojia ya uandishi na habari yamewawezesha wanajamii kuzikusanya na kusiwasilisha, kuzisambaza na kuzihifadhi kwa kutumia vifaa hivyo. Utumiaji wa teknolojia hizi kwa upande mmoja yamewezesha kuziendeleza na kuzidumisha ngano zilizomo katika jamii ya Wazanzibar. Kwa upande mwengine, zinaonekana kuvizwa kutokana na ukweli kuwa wengi wanaofaidika ni wasomi.

## 5.3 Matokeo ya utafiti

Utafiti huu umedhihirisha kuwa kuna mabadiliko chanya na hasi katika kuzitunga, kuziwasilisha, kuzisambaza, kuzihifadhi na hata dhima za ngano hizo kwa kutumia teknolojia kama vile kompyuta, CD, vinasa sauti na maandishi. Ngano hapo zamani kabla ya majilio ya wageni ambao walileta teknolojia ya uandishi zilikuwa na mifumo yake katika utungaji, uwasilishaji, uhifadhi na usambazaji wake. Kwa upande wa utungaji ulikuwa ni wa papo kwa papo. Fanani alibadilisha maudhui ya ngano kutokana na muktadha na hali iliyopo wakati wa usimuliaji. Uwasilishwaji ulikuwa ni kwa njia ya mdomo, ambapo fanani na hadhira walionana na kushirikiana katika baadhi ya matendo. Wasimuliaji walikuwa ni watu wazima, na walengwa walikuwa ni watoto wanaokisiwa kuwa na umri wa miaka mitano hadi kumi na saba.

Uhifadhi ulikuwa ni wa moyoni na kichwani. Usambazaji ulifanywa kwa njia ya masimulizi; hii ni njia ambayo ilitumika kuzirithisha kutaka kizazi kimoja hadi kingine. Aidha dhima za ngano zilikuwa ni kuasa, kurekebisha, kuadilisha, kurithisha amali za kijamii na kuburudisha.

Vile vile, kutokana na maendeleo ya teknolojia iliyomo katika jamii, kuna vifaa mbali mbali vinavyotumika kuwasilishia, kuhifadhi na kusambaza ngano. Vifaa hivi kwa kiasi kikubwa vimeleta mabadiliko katika utanzu huu wa fasihi simulizi. Miongani mwa teknolojia inayotumika  ni kama vile CD,kompyuta, kanda za video na TV, kanda za kunasia sauti na redio na maandishi. Viasa sauti, kanda za video na CD, huambatana na redio au TV kurusha ngano. Kompyuta hutmia program maalum kuzihifadhi na mtu akizihitaji hupaswa kufungua hiyo program na kuzisoma. Katika maandishi zinaonekana katika vitabu.

Athari ambazo zimejitokeza kutokana na utumiaji wa teknolojia zilizoainishwa, zimegawika katika makundi mawili. Kwanza ni athari chanya; hizi ni athari ambazo zinaziendeleza ngano. Miongoni mwa athari chanya zilizojitokeza ni kudumu kwa muda mrefu hasa kupitia mandishi na kopyuta, kutumika kama nyenzo ya kufundishia lugha maskulini, zinasambaa katika eneo kubwa kwani vifaa hivyo hutumiwa na watu walio wengi na kuhifadhi utamaduni wa jamii. Pili ni athari hasi; Haya ni matokeo yanayoonesha kuziviza ngano teknolojia za kisasa zinapotumika kuhifadhia, kusambaza na kuwasilishia ngano. Miongoni mwa athari hizo ni kupoteza uhalisi wake kwa vile zinapowasilishwa baadhi ya mambo hukosekana. Kama vile kukosekana ushiriki wa hadhira, fanani na hadhira huwa hawaonani, kukosekana usimulizi na baadhi ya ishara kukosekana. Pia kuna athari ya kupotea kwa ngano zilizohifadhiwa kwani baadhi ya vifaa hivyo hupotea au kuharibika, kufa

kwa utamaduni wa kutoleana na kusikiliza ngano, kupata umbo la kudumu; kwa hiyo muktadha na mazingira hayana nafasi katika uwasilishaji wa ngano na pia kufaidika watu wachache kwa sabau baadhi ya vifaa hivyo ni ghali na vinahitaji utaalamu.

**5.4 Mapendekezo ya Utafiti**

Kutokana na matokeo ya utafiti yalivyoonesha, mtafiti ametoa mapendekezo yafutayo kwa jamii na wapenzi wa fasihi:

i) Serikati, kupitia Wizara ya Utamaduni kuchukua jukumu la kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa ngano katika jamii. Vile vile wizara kuzikusanya ngano kwa ajili ya kuzihifadhi ili zisipotee moja kwa moja kwa sababu ya kuzuka kwa teknolojia hizo.

ii) Kuwe na utaratibu wa kuzikusanya na kuzihifadhi katika teknolojia ya kudumu zaidi, ikiwezekana kuziwasilisha kwa njia ya michezo ya kuigiza ili watoto na watu wazima waweze kuzifatilia na kuziangalia ili kupata uasili wake uliomo katika ngano hizo.

iii) Wizara ya Elimu isizitumie ngano kwa kufundishia sarufi ya lugha tu, bali wazitumie kama ni nyenzo ya kuwapa watoto taaluma ambayo imo katika ngano hizo. Hili litawezesha watoto kujengeka kimaadili na wataweza kuzihifadhi.

**5.5 Mapendekezo Kuhusu tafiti Nyengine:**

Baada ya kupata matokeo hayo, mtafiti wa utafiti huu ametoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wengine wa fasihi:

i) Licha ya kuwa tafiti nyingi zimefanywa kuhusiana na ngano, nafasi ya mwanamke katika ngano haijaangaliwa. Hivyo tafiti zijazo zijadili nafasi ya mwanamke katika ngano.

ii) Utafiti mwengine ujikite katika kuwaangalia wahusika na nafasi zao.

iii) Tofauti ya kimitindo katika utungaji wa ngano. Kama zilivyokawaida ya kazi za faihi kuundwa kwa mitindo mbali mbali, ngano nazo zina mitindo ambayo bado haijashughulikiwa.

## MAREJELEO


Eagleton,T (1983) *Literary Theory: An Introduction*. Blackwell, London.

Else, D (1993) *Guide to Zanzibar and Pemba*. UK, Bradt Publications. International Publishers

Finnegan, R (1970) *Oral Literature in Africa*. Clarrendon Press, Oxford.

Ingrams, W.H (1967) *Zanzibar Its History and Its People.* Frank Class & Co LTD.

Juma , Kh na wenzake (2008) *Utamaduni wa Mzanzibar*. Zanzibar, BAKIZA.

Kezilahabi, E (1995) Siasa, Teknolojia na Ukuaji wa Fasihi ya Kiswahili katika *Kioo cha Lugha* Juzuu ya 1, Daressalaam.

Khamis, A. A na wenzake (2008) *Utamaduni wa Mzanzibar.* Zanzibar, BAKIZA.

Kothari, C.R (2009) *Research Methodology; Methods and Techniques*. Vishwaprakash, New Deihi.

Madumulla, J.S (2009) *Riwaya ya Kiswahili; Nadharia, Historian a Misingi ya Uchambuzi.* Tanzania, Mture Education Publisher Ltd.

Mbunda , M (1992) *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es salaam, Educational Publishers Ltd.

Mdee, J. S na Mrikaria, G (2006) Nadharia ya Fasihi Simulizi na Maendeleo katika Sayansi Teknolojia katika *Mulika* Juzuu 27 Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dae es salaam.

Mulokozi, M.M (1996) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili; OSW 105: Fasihi ya Kiswahili*.

Mushengyezi, A (2003) *Twentieth Century Literary Theory.* Deoartment of Distance Education, Kampala.

Mutembei, A (2005) Uwasilishwaji, Uhufadhi na Usambazaji Fasihi Simulizi hapo Kale na Sasa katika *Mulika* Vol 27: 11 TUKI.

Oxford (2000) *Advanced Learners Dictionary of current English*. Nairobi, Oxford University Press.

Rajmund, O (1991) *Aggressive Prose, A Case Study in Kiswahili Prose*. Dar es salaam, Institu of Kiswahili and Research.

Senkoro, F.E.M.K (2011) *Fasihi.* Daressalaam, KAUTTU Limited.

Simiyu, W.F (2011) *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Mwanza Tanzania, Serengeti Bookshop.

Songoyi, E. M (1997) *OLT 103 1: Oral Literature 1*. Daressalaam, Open University of Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania (1996) *Kiswahili Kidato cha Nne: Kitabu cha Mwanafunzi.* Daressalaam, Oxford Univwesity Press.

Wamitila, K. W (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Kenya, Focus Publication.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (2006) *Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Kwanza*. Dar es Salaam, Oxford University Press. WWW. Shuledirect. Co.tz.

## VIAMBATANISHO

### Hadithi Zilizotumika

### Kiambatanisho 1: Hadithi ya jongoo na nyoka

Msimuliaji: Paukwa

Wasikilizaji: Pakawa

Msamuliaji: Hapo zamani za kale alikuwapo jongoo na nyoka. Jongoo alijaaliwa kuwa na macho. Nyoka yeye alijaaliwa kuwa na miguu. Wanyama hawa walikuwa marafiki sana. Kila mmoja alimpenda mwenzake, hivyo waliishi kama ndugu.Walisaidiana kwa raha na shida. Siku moja nyoka alialikwa harusi na jirani yao. Nyoka alitaka kwenda harusini; jongoo naye alitaka kuhudhuria. Nyoka akaanza kulalamika "ah! ningekuwa na macho ningekwenda kuona kila kitu. Afadhali wewe mwenzangu unaona, angalau ungeniazima rafiki yangu; Jongoo naye akajibu mimi pia naomba Mwenyezi Mungu angelijaalia miguu kama wewe, ningeweza kutembea masafa marefu, na huko harusini nisingepata shida ya kufika. Nyoka kusikia hivyo haraka haraka akasimama na kumwambia jongoo; "Basi mimi nikupe miguu na wewe uniazime macho yako tutakaporejea nitakurudishia macho yako na mimi utanipa miguu yangu, wanaje shauri langu?" Jongoo bila ya kufikiri aliitikia kwa furaha. Aliona ,.miguu itamsaidia kila kitu. Akakubali. Nyoka naye kwa shauku aliyokuwa nayo akapokea macho ya jongoo haraka haraka, na yeye kumkabidhi jongoo miguu bila ajizi.

Walivyorudi harusini nyoka alikimbia na hakurudi tena kumrejeshea jongoo macho yake na yeye kuchukua miguu yake. Hii ndio maana jongoo mpaka leo anamtafuta nyoka amrejeshee macho yake naye ampe miguu yake.

**Msimuliaji**: Bi Aziza Khamis (Mwanyanya Zanzibar)

**Kiambatanisho 2: Hadithi ya Mnara wa Baba na Mama**

Paukwa………………Pakawa!

Hapo zamani za kale alikuwapo mwanamme aliyeoa na kuzaa mtoto mmoja wa kike. Akakaa baadae akaoa mke mwengine; hivyo wakawa mtu na mkemwenziwe. Mke mdogo alikuwa mfinyanzi; alifinyanga vyungu, vikombe na mikungu. Mke wa pili naye kwa bahati alizaa mtoto wa kike. Mtoto wa mke wa kwanza alimuona ndugu yake akichezea vyombo alivyotengezewa na mama yake. Siku moja, yule mtoto wa kwanza akenda kwa mama yake na kumwambia “mama na mimi nataka mkungu na kijungu.” Mama yake akamjibu “Mimi sijui kufinyanga.” Yule mtoto akauliza “Mbona ndugu yangu anavyo?” Mama akamjibu “Yeye hutengenezewa na mama yake.”

Yule mtoto akatoka mbio hadi kwa mama yake wa kambo. Alipofika akamwambia mama yake wa kambo “Mama na mimi nataka kijungu na mkugu.” Yule mama alimwitikia na kukubali kwa masharti ya kuwa Yule mtoto ende akamuue mama yake. Mtoto akakubali lakini akajibu “Nitamuua vipi mama name sjui?” Yule mama akamfundisha jinsi ya kumuua. Akamwambia kuwa ikifika saa sita mchana amuombe mama yake kuoga; kuoga kwenyewe kuwe kisimani. Atakapoinama kuchota maji amsukume kisimani, akiweza hivyo atatengezewa kijungu na mkungu.

Mtoto kusikia vile alitoka mpaka kwa mama yake. Ilipofika saa sita, mtoto akalia huku akisema “Mama naona joto, nataka kuoga.” Mama akamnasihi mtoto wake achote maji ndani akakoge, lakini wapi! Mtoto alikataa katakata na kutaka akakogeshwe kisimani. Mama kuona mwanawe ameng’ang’nia alimchukua hadi kisimani. Walipofika kisimani yule mama alikwenda kuchota maji. Wakati ameinama kuchota maji, mtoto alimsogelea na kumsukumiza ndani ya kisima.

Baada ya kumtumbukiza mama yake kisimani alikimbia mbio huku akiwa na furaha ya kuwa matarajio ya kupata kijungu na mkungu yametimia. Alipofika kwa mama yake wa kambo alimueleza kuwa tayari keshamuua mama yake. Mama kusikia hivyo alimjia juu na kumwambia “Wewe mtoto mbaya sana. Umemuua mama yako? Kumbe wewe mtoto hasidi, sitaki hata kukuona na utoke sasa hivi.” Mtoto kusikia maneno hayo alilia sana. Kuazia hapo akaanza kunyimwa chakula hadi malazi. Mtoto aliondoka na kilio hadi kwao. Alipofika, nyumba ilkuwa imefungwa. Akalala nje chini ya kizingiti huku akilia mpaka usingizi ulipomchukua.

Wakati amelala, usingizini akamuona mama yake amekuja. Alipofika akamwambia “Mwanangu usilie haya umeyataka mwenyewe. Kule mwituni kwenye konde yetu, mimi na baba yako tuna ng’ombe nenda na ukifika immba; ng’ombe wa baba na mama fungua mlango nipite!  Atakapofungua mdomo wake utapita, humo utalishwa na kuvishwa. Hutapata shida mwanangu, usihuzunike.” Yule mtoto kulipokucha alikwenda mpaka yule ng’ombe , alimkaribia akaimba;

*Ng’ombe wa baba na mama fungua mlango nipitee!*

Yule ng’ombe akalia “Baa!” ulipofunguka mdomo, mtoto aliingia tumboni mwa ng’ombe. Alipofika humo alikogeshwa, akapewa nguo na akapewa chakula. Alipotoka alikuwa mzuri! Mwendo huu uliendelea kwa muda mrefu. Mama yalimtaajabisha sana na mambo yale. Hakujua mi wapi anapovipata vitu vile.Yule mama na mtoto wake walianza kumshuku kuwa anakwenda akiiba. Siku moja yule mama akamwambia mtoto wake amfuate dada yake ajue anakokwenda kuuba vitu vile. Mtoto akafanya kama alivyoambiwa na mama yake. Alimfuata dada yake bila yeye mwenyewe kufahamu kuwa kuna mtu anamfuata. Alipofika ile sehemu alisema

yale maneo na ng’ombe akafunua mdomo wake naye akaingia. Mtoto kuona vile alirudi mbio nyumbani na kumueleza mama yake kila kitu. Mama choyo kikamjaa.

Aliporudi mume wake, alijifanya mgonjwa. Chini ya kitanda aliweka maganda ya kombe na juu akaweka mkeka. Katika ugonjwa huo kama akigeuza ubavu wakati amelala, zile kombe zilitatalika. Zinapotatalika yeye ndio hujifanya mgonjwa zaidi na kusema mgongo unaalika. Maganga yakesha ugonjwa haukupona. Siku moja alipoamka akamwambia mumewe kuwa ameoteshwa kuwa kule kondeni kuna ng’ombe ni lazima achinjwe itolewe sadaka ndipo ugonjwa utapona. Ng’ombe alichinjwa. Watu wakaalikwa kuja kula karamu.

Baada ya ng’ombe kuchinjwa mtoto ikawa hana pa kwenda. Wakati amelala mama yake akaja tena na kumwambia “Mwanangu usilie haya umeyataka mwenyewe. Ninachokusihi usile nyama ya huyo ng’ombe. Wewe chukua mifupa, itie kwenye pakacha na wende ukaitupe pwani.” Wakati wa karamu ile yule mtoto hakula ile nyama watu wakawa wanamshangaa na kuoneshana; alichukua ile mifupa na kwenda kuitupa pwani.

Kule pwani baada ya kumwagwa mifupa kuliota mnara. Watu wakauona na kuanza kuushangaa. Mbiu ya mgambo ikapigwa, watu kutoka sehemu mbalimbali walitoka kwenda kuuona ule mnara. Mama akamuosha mtoto wake wakenda kuuangalia mnara. Yule mtoto maskini! alivishwa vitambara na kuwekwa jikoni, kupakwa masinzi na akaambiwa asitoke. Kule pwani watu waliufurahia mnara ule na kuuita uje ufukweni, lakini wapi! Mnara haukusogea. Majirani walishangaa; jogoo ambaye alikuwa kaka pembeni akawika;

*Ko ko ikooo! Mwenye mnara hayupo.*

Jogoo alifukuzwa lakini hakuondoka akaendelea kuika. Watu wakaanza kuulizana "Hivi ni nani aliyekuwa hayupo?" Katika kufanya uchunguzi,baba akagundua kuwa ni yule mwanawe. Akamuuliza mkewe yuko wapi, mama akajibu kuwa amekataa mwenyewe kuja. Baba akamwambia ende akamchukue akataa. Baba akatoka akenda kumchukua. Mtoto alipofika akaanza kuimba:

*Mnara wa baba na mama njoo pwani njoo!*

*Mnara wa baba na mama njoo pwani njoo!*

Mara ule mnara ukasogea hadi ukamgusa yule mtoo ukamchukua. Ndani ya mnara alikuwamo mfalme. Ikafungwa ndoa hapo hapo ufukweni; hivyo akawa mke wa mfalme. Maisha yakawa mazuri. Mfalme akawajengea wazee wa mke wake jumba la thamani. Wakapatiwa kila wlichokihitaji; wakaishi maisha mazuri.

Mama wa kambo yalimkera sana mambo yale. Akatamani mwanawe ndio aolewe na mfalme.Hivyo akapanga njama nyengine za kumkandamiza yule mtoto. Akamwambia mwanawe nenda kamuangalie dada yako. Akampa sindano saba, akamwambia "Ukifika muombe umsuke, utakapomsuka mchome hizi sindano." Mtoto akatoka hadi kwa dada yake na alipofika akamwambia leo nimekuja kukuangalia. Yule dada akafurahi kumsikia ndugu yake. Baada ya kula alimwambia "dada njoo nikusuke" Yule dada alikataa. Ndugu yule alishikilia hadi dada akakubali. Wakati anachana alimchoma sindano ya kwanza, dada akauliza "unanichoma nini", naywe akajibu " sikuchomi kitu nimebanja chawa tu." Mtoto alimchoma dada yake sindano hadi zikamalizika. Sindano ya mwisho Yule dada akgeuka kuwa ndege mzuri sana akaruka. Mara tu baada ya ndege kuruka nyumbailbadilika, ile nuru iliokuwemo ikaondoka. Mfalme aliporudi akaona

mabadiliko; akaanza kuita “ mke wangu uko wapi?, mbona leo kuna kiza humu ndani?” Yule mtoto akajibu “mimi niko huku, hakuna kitu.” Mfalme kusikia ile sauti akajua kuwa yule siye mke wake.

Ndani ya nyumba ile kuna bustani ambayo ndani yake kuna mtama, uwele na aina nyengine za nafaka. Mule ndani ya nyumba kulikuwa na kibaraka ambaye alikuwa anashughulikia bustani. Ilipofika jioni yule ndege akaja kwenye bustani na kuimba:

Ndege: Kibaraka kibaraka
Kibaraka: labee bibi labee
Ndege: Nile mtama nisile
Kibaraka: kula bibi kula
Ndege: Nile uwele nisile
Kibaraka: Kula bibi kula
Ndege: Baba yako kenda wapi
Kibaraka: Kenda msikitini kusali na kuadhini
Ndege: Akija nisalimiee!

Kwa muda wa siku tatu ndege yule alikuja na kuimba, anakula akimaliza anaruka. Siku ya tatu yule kibaraka akamueleza bwana wake. Baada ya mfalme kuelezwa vile, alitayarisha urimbo kwa ajili ya kumtega yule ndege. Ulipofika wakati wa jioni, mfalme alijitegesha mahali na kusubiri. Ndege alikuja na kuanza kuimba. Alipotaka kuruka hakuweza; mbawa zake zilinasa kwenye urimbo. Mfalme aliamuru ndege kukamatwa. Kibaraka alimpelekea, mfalme alianza kumpapasa yule ndege. Wakati akifanya hivyo, alishangazwa kuona amekuta sindano mwilini mwake. Aliendelea kumpapasa mpaka ilipofika sindano ya saba, yule ndege aligeuka na kurudi katika hali yake ya ubinadamu.

Mfalme alipigwa na butwaa kumuona mke wake. Nuru ya nyumba ilirejea; nyumba ikang’ara kama awali. Kule ndani yule ndugu aliyemfanyia dada yake uovu ule alikwenda kuchukuliwa na kuletwa mbele ya mfalme. Alipofika, alitakiwa kueleza kwa nini amefanya vile. Mfalme alikasirika sana kwa uadui ule. Alimchinja yule binti, ikaandaliwa karamu. Watu walioalikwa walichinjiwa ng’ombe. Wazazi wa yule mtoto walialikwa, wakahudhuria. Ilipofika wakati wa kula, mama mkwe alipakuliwa sahani yake. Akatayarishiwa kila kitu kinachostahiki. Wakati anaendele kula jogoo alisogea na kuika;

*Ko ko ikoo! Kuna mmoja ala chongo la mwanawe.*

Watu wakashughulika kumfukuza jogoo; lakini wapi! Hakuondoka, aliendelea na wimbo wake. Mama alipofika katikati ya sahani alishangaa kuona jicho la mtu; jicho la mwanawe. Alianguka chini na kupoteza fahamu. Alipozinduka, mfalme akamuhoji kwa nini aliamua kufanyia uovu ule. Ikambidi kueleza tokea alivyofanya mpaka mtoto akamtumbukiza mama yake mule kisimani, namna alivyojitia kuumwa ng’ombe akachinjwa na hila yake ya kutaka kumuangamiza mwanawe wa kambo. Kusikia hayo mfalme. Baba wa mtoto na takriban watu wote waliohudhuria pale walichukizwa na matendo yale.  Mfalme akaamua kumuhamisha katika nyumba alizozijenga, baba akamuacha kwa kuuliwa mke wake na kutesewa mtoto wake. Baadae mfalme akaamua kumchukua mkwe wake wa kiume na kuishi naye pamoja.

**Chanzo:** Bi Sharifa- Mtoni Zanziba

**Kiambatanisho 3: Hadithi ya Mtendazema**

Paukwa!   Pakawa

Hapo kale alikuwepo mfalme na mkewe waliopendana sana lakini hawakuzaa kwa muda mrefu. Mwisho walipata watoto wawili wa kiume uzeeni. Watoto hao walilelewa kama kawaida ya watoto wa kifalme mpaka wakawa wakubwa kidogo. Kila mmoja alikuwa na mlezi wake. Wakati wa jioni walezi huwachukua watoto hao wakaenda kutembea.

Katika mji wa mfalme huyo alikuwepo mshoni jina lake Mtendazema. Walezi pamoja na watoto wao lazima kila siku wapiti kwa Mtendazema kumtazama. Wakifika humwita ‘Mtendazema’ naye anajibu ‘Naam mtendazema hutendea nafsi yake, na mtendaziovu hutenda nafsi yake.’ Walezi hucheka sana kasha kuendelea na safari yao.

Desturi hiyo iliendelea kwa muda mrefu sana hata watoto wa mfalme wakawa wakubwa, wanaweza kutembea wenyewe bila kufuatwa na mtu.

Watoto wakitoka hawendi kutembea popote ila kwa Mtendazema. Wakifita humpigia kelele ‘ Ba Mtendazema’ naye hujibu ‘Naam Babu! Mtendazema hutendea nafsi yake na mtendaziovu hutendea nafsi yake.’ Wakisikia hivyo  watoto hufurahi sana kasha hukaa papo hapo na kucheza. Mtendazema aliwafanyia desturi ya kuwaekea kitu chochote cha kula kama njugu, ndizi, embe, viazi vya kuchemsha au muhogo.

Watoto wanaporudi kwa malkia huwauliza ‘Huwa munakwenda wapi kucheza? Watoto kwa

furaha humjibu sisi hatwendi pahala popote ila kwa Ba Mtendazema. Tukienda sisi huita ‘Ba Mtendazema’ Ba Mtendazema! Yeye hujibu kuwa mtendazema hutendea nafsi yake na mtendaziovu hutendea nafsi yake.

Kuwasikia watoto wake hivyo. Malkia aliudhika sana na akasema ‘Mtendazema, anatenda gani: tutamwona huo wema wake atakaoutenda!’

Desturi iyo iliendelea kwa muda mrefu sana hata mwisho Malkia akawaza bora amuue Mtendazema, siku hiyo akafanya mkate wa mayai, akautia sumu kasha akampa mtumishi wake ampelekee Mtendazema. Mtendazema alipopelekewa mkate na mtumishi wa Malkia alifurahi sana, akaupokea na akauweka juu ya meza yake. Jioni siku hiyo hiyo watoto walikwenda kuzungumza kwa rafiki yao. Walipofka walimkuta juu ya cherahani yake anashona nguo. Pia wapo watu waliokuja kuleta nguo zao kushonewa.

Siku ile Mtendazema hakuwa na chochote cha kuwapa ila mkate ule ule ulioletwa na Malkia.Kwa hiyo, aliuchukua mkate na kuukata vipande vitatu: viwili akawagaia wale watoto, kimoja akakiweka akimaliza kazi yake ale. Watoto baada ya kuula mkate walianza kulalamika kwa tumbo linavyouma. Hawakukaa tena, walimuaga Mtendazema wakenda zao kwao. Walipofika walianza kutapika damu. Malkia aliwauliza kitu gani walichokula.

Walisema hawakula chochote ila mkate wa mayai waliopewa na Mtendazema. Malkia kusikia vile mbio alimwita mfalme akamwambia “Njoo bwana uone mambo! Watoto walikwenda kwa Mtendazema wakapewa mkate. Mkate kula, wamerudi tizama hali hii.” Si muda mkubwa watoto walianguka wakafa.

Mfalme akawatuma askari wakamchukue Mtendazema na mkate wake. Bila ya ukaidi Mtendazema akawafuata, mfalme alimuuliza kitu alichowapa wanawe hata wakafa. Mtendazema aliingiwa na hofu kubwa huku akitetemeka akamjibu kwa unyenyekevu mfalme kuwa hakuwapa kitu chochote ila mkate wa mayai ambao alipewa na Malkia.

Mfalme akatoa amri ya kuitwa daktari na kuuchunguza mkate. Kwa bahati mkate ulionekana na sumu.

Mfalme akamwita Malkia akamwambia ‘Nini dhamiri yako kupika mkate ukautia sumu kisha ukampelekea Mtendazema? Kama dhamiri yako ni kumuua Mtendazema basi jina alilojipa limesibu. Mtendazema hutendea nafsi yake na mtendaziovu hutendea nafsi yake. Kwa hiyo uovu uliomtendea Mtendazema umekurudia mwenyewe kwani umewaua watoto wote wawili kwa wakati mmoja.

Mfalme alitayrisha maziko akawazika watoto wake. Mtendazema akahama mji ule na Malkia akashonea fumba akatoswa baharini.

**Chanzo:** *Fasihi Simulizi Zanzibar* (1983: 80- 82)

**Kiambatanisho 4: Hadithi ya Zimwi**

Paukwa………..Pakawa!

Aliondokea mtu na mkewe ambao walibahatika kupata mtoto mmoja wa kike. Walimlea mtoto wao katoka maadili mema. Mtoto aliwaheshimu watu wote; wakubwa kwa wadogo.Wazazi walimpenda sana mtoto wao. Ijapokuwa walikuwa maskini; walijitahidi kumridhisha mtoto wao kwa kila alichokihitaji. Katika mtaa huo alikuwapo zimwi ambaye alikuwa anaonekana kujishughulisha sana kusoma kur-an. Mtoto alipofikia umri wa kusoma alipelekwa chuoni. Mwalimu alikuwa ni zimwi. Mtoto alisoma kwa hima. Siku moja, mwalimu alimwambi yule mtoto amletee yai la kuku kama ujira wa kumsomesha. Mtoto alipofika nyumbani. Kwa shauku alianza kuimba:

*Mwalimu kataka yai la kuandikia*
*Mwalimu kataka yai la kuandikia*

Kutokana na kuwa mama alitaka kumridhisha mwanawe alimjibu:

*Mpe yaya mpe,*
*Mpe yaya mpe,*
*Mwanafunzi wa kwanza dawa,*
*Mpe yaya mpe!*

Yule mtoto kulikuwa na kuku ametaga kwa hiyo akalichukua yai na kumpelekea.Yule zimwi alilila lile yai. Mwanafunzi akaendelea kwenda chuoni. Baada ya masiku kupita yule zimwi akamwambia yule mtoto nenda kaniletee kuku. Mtoto akatoka hadi kwa mama yake na kuimba:

*Mwalimu kataka kuku wa kuandikia,*
*Mwaalimu kataka kuku wa kuandikia*

Mama akamjibu

*Mpe yaya mpe,*

*Mpe yaya mpe,*

*Mwanafunzi wa kwanza dawa*

*Mpe yaya mpe!*

Zimwi kutokana na tamaa yake akaona kapata sehemu ya kushibisha njaa yake. Mara kamdai hiki mara kile. Ikafika wakati ikawa hata baa yake na mama yake wameshaliwa. Hapo mtoto alioondoka katika kijiji hicho na kukimbilia asikokujua. Alikuwa kabakia peke yake; hana baba wala mama. Akafika katika kijiji chengine ambako watu waliishi vizuri. Kutokana na uzuri wake na tabia zake njema alipendeza kwa watu wote pale kijijini. Akapelekwa kwa mfalme kama mtumishi. Alikaa hapo kwa muda mrefu. Mfalme alikuwa na mtoto wake wa kiume ambaye aliondokea kumpenda binti huyo. Mfalme alilikubali shauri la mwanawe na kwa hiyo akaozeshwa. Yule msichana akamueleza mumewe mambo yaliyompata. Yule kijana alitoka na kwenda kumtafuta zimwi kupigana naye. Alipompata alimpiga hadi akaaga dunia. Akarudi na kuishi na mke wake raha mutarehe.

**Chanzo:** Bi Fatma Khamis- Mwanyanya.

**Kiambatanisho 5: Hadithi ya Sungura na Buyu la Asali**

Paukwa.....................Pakawa!

Hapo zamani palitokea dhiki kubwa. Siku moja, sungura alikwenda kutafuta chakula. Alipofika msituni aliona mbuyu mkubwa sana. Alipoyatupa macho yake juu, aliona mzinga wa nyuki. Aliamua kurudi nyumbani ili awaite wenzake waje kula asali. Alipita na kumwambia panyabuku; “Baba ameaga dunia na ameniachia mzinga wa asali. “Twende tukale”. Wote waliondoka kuelekea mwituni. Walipofika huko, sungura alimwambia mwenzake; “panda juu”. Panyabuku alifanya hivyo. Sungura naye alimfuata. Walikuwa na mienge ya moto. Waliwachoma nyuki mzingani. Walianza kula asali. Mara alitokea simba. Aliyatupa macho yake juu na kumuona sungura na panyabuku wanakula asali. Aliwauliza,“Nyinyi ni nani?” Sungura akamwambia panyabuku: “Nyamaza ana wazimu mzee yule!” Simba aliuliza tena “Nani nyinyi, hamsemi?” Panyabuku aliogopa baada ya kusikia ile sauti nzito ya simba, akajibu; “sisi hapa.” Sungura alimwambia panyabuku; “Nitwae na unitie kwenye mwenge. Umwambie mzee simba, jitenge nitupe mwenge. Nami ninakuja” Panya alifanya kama alivyoambiwa. Alipomtajia, simba alijitenga. Panyabuku aliutupa mwenge chini. Ulipoanguka, sungura alifyatuka kama mshale. Huyoo alikimbia, akaenda zake. Simba alimwambia panyabuku, “shuka haraka.” Panyabuku alishuka kwa hofu kubwa. Alipofika chini tu, simba alimkamata na kumla. Baadae alitoka kwenda kumtafuta sungura, asimwone.

Baada ya siku kadhaa sungura alikwenda kwa kobe. Alimwita na kumdanganya kama panyabuku. Sungura na kobe walikaa kitako na kuanza kula asali. Mara alitokea simba mwenye

mzinga wa asali. Aliuliza, “Nani nyinyi juu?” Sungura alimwambia kobe; “Nyamaza!” Simba alitulia na baada ya muda aliuliza tena. Kobe aliingiwa na hofu, alimwambia sungura; “Mimi nasema. Umeniambia asali ni yako, bali ya simba!” Simba aliuliza tena: “Nani nyinyi?” Kobe alimwambia; “Sisi hapa Simba alisema kwa sauti nzito; “Haya shukeni haraka.” Kobe alisema; “Tutakuja” Simba aliyemkosa kwa siku nyingi alijisemea; “Leo nitampata sungura. Sugura alimwambia kobe kama alivyomwambia panyabuku. Kobe alijibu; “Vyema” Moyoni mwake alijisemea; Huyu anataka kukimbia aniache mimi niliwe na simba! Ataliwa yeye kwanza” Alimtwaa sungura na kumtia ndani ya mwenge kama alivyosema. Alimwambia simba, “Sungura huyo anakuja!” Simba alimdaka haraka na kumla.

**Chanzo**: *Kiswahili Kitabu cha mwanafunzi darasa la tatu, Zanzibar* (2006: 50- 51)

**Kiambatanisho 6: Kinyonga Mfalme wa Wanyama**

Hadithi hadithi……….. Hadithi njoo!

Hapo zamani za kale wanyama waliishi pamoja na kupendana. Kila mmoja alimjali mwenzake. Simba alikuwa ni mfalme wa wanyama wote. Simba aliyatumia madaraka yake kuwaonea wananchi wake huko msituni. Aliwaonea wanyama wengine kutokana na ubabe wake. Aliwaonea wanyama dhaifu kama vile swala, pundamilia, nyati na wengineo. Hali hii iliwasononesha sana wanyama wengine. Walikuwa hawana raha ya kutoka na kutembea. Ndipo siku hiyo wakakaa na kuzungumza juu ya hatima yao. Ikaamuliwa kupitishwa uchaguzi wa kuchagua kiongozi mwengine. Kiti cha ufalme kiliwekwa, na baadae ikaamuliwa wanyama wote

waondoke kwenda katika uwanja. Walipofika huko uamuzi ukatoka kuwa kuwe na mashindano ya mbio. Mnyama ambaye atafika mwanzo kwenye kiti na kukikalia ndiye ambaye atashika madaraka na kuwa mfalme. Ushauri ukakubaliwa na wanyama wote. Kinyonga ambaye mwendo wake ni wa polepole, hakuwa na uwezo wa kukimbia haraka kama wanyama wengine.

Kinyonga alijikongoja akichapia matawi ya miti kuelekea kwenye kiti. Kadiri alivyojitahidi hakuweza kuwashinda wanyama wengine. Kutokana na umbile lake, alijigeuza rangi ya kijani na kujiweka nchani mwa tawi lililokaribu na njia. Alifanya hivyo ili akipita mnyama wa mwanzo aweze kujitia mkiani mwake ili afike mwanzo. Kwa bahati paa akawa mnyama wa kwanza kupita. Alijirusha na kujifunga katika mkia wa paa. Walipofika paa aliruka kutaka kukalia kiti.

Ghafla kinyonga alilia na kusema “Unaniumiza huoni kama kuna mwezio ameshafika!” Paa kusikia vile aliruka na kukaa upande akisikitika kwa kukosa ufalme. Alimuomba radhi kinyonga. Kinyonga alikubali.

Wanyama wengine walipofika walishangaa kumuona kinyonga amekalia kiti cha ufalme. Wako ambao walimpongeza kwa ushujaa wake, lakini paa aliishiwa nguvu kwa tukio lile. Tangu siku hiyo kinyonga akawa mfalme wa wanyama.

**Chanzo:** Bi Sharifa

## Kiambatanisho 7: Hadithi ya Mcheka Kilema

Hadithi hadithi ……………Hadithi njoo!

Hapo zamani za kale alikuwapo bibi ambaye alikuwa mlemavu. Chuchu lake moja lilikuwa kubwa, akitembea linaburutika chini. Bibihuyo alikuwa na mtoto wake wa kike ambaye alishakuwa kigori. Bibi alikuwa ni maskini, mume wake alishafariki, kwa hivyo alijishughulisha na kilimo.Yeye na mtomto wake walikuwa wanakwenda shamba kulima mpunga na mihogo ili kupata angalau chakula. Mto aliendelea kuwa mkubwa mpaka akavunja ungo. Kuna siku mama yake alichelewa kurudi kutoka kondeni, hivyo yeyeakarudi kwenda kutayarisha chakula. Mara ikabishwa hodi. Mtoto akatoka. Alipofungua mlango alikutakijana wa kiume. Kwa hofu mtoto alitaka kufunga mlango. Yule kaka akamueleza “usiogope, mimi nimekuja kutafuta mchumba nataka nikuoe.” Yule msichana kusikia hivyo alimwambia yule kijana “subiri nikamwite mama yangu.” Yule msichana akenda na furaha, na alipofika akamweleza mama yake huku akiimba

Mama njoo, Mama njoo,
nyumbani kumeingia wageni
Mama njoo!

Yule bibi akaburuta chuchu lakle huku akiimba

Mwanangu, mwanangu, mwanangu
Mcheka kilema si mkwe wangu
Mwananguuu,
Chuchu bingiri bingiri
Seka hamuone mkwe wangu!

Yule bibi akaburuta chuchu lake na kwenda nyumbani. Yule mvulana alipomuona yule bibi namna anavyotembea hakuweza kujizuia, alicheka sana; Yule bibi akasema

“Wewe hunifai toka nenda zako.” Yule kijana akaondoka lakini bado hajaamini kwamba amemkosa mwanamke . Baada ya masiku kupita, alikuja kijana mwengine kwa azma hiyo hiyo. Yule bibi akasema tena kama mwanzo. Na huyu pia hakuweza kujizuia. Naye asipate kumuoa Yule mwanamke. Bibi na mwanawe wakaendelea kuishi katika hali yao ya umaskini. Hata siku moja akatokea mtoto mzuri wa kiume. Alipofika akakaribishwa. Yule msichana akenda kumwita mama yake. Yule mama akajiburuta huku akiimba nyimbo yake. Alipofika alimuona yule kijana amekaa. Kijana aliinuka kwa heshima na kumsaidia yule mama huku akimwambia “pole mama.” Yule mama baada ya kwisha kukaa akamuuliza Yule kijana “Nieleze shida yako ee mwanangu.” kwa upole na heshima alieleza shida yake. Basi mama alifurahi na kumwambia binti yake “ Huyu ndiye mume anayefaa kukuoa.” Mtoto akakubali alivyoambiwa na mama yake. Harusi ikapangwa; wazee wa mtoto wa kiume wakapeleka posa na harusi ikafanywa. Wawili hao waliishi raha mustarehe pamoja na mama yao.

**Msimuliaji:** Bw. Muhammed (Mwanyanya)